# KUCHUNGUZA USAWIRI CHANYA WA MWANAMKE KATIKA VITENDAWILI VYA JAMII YA WANYIHA

**MSHANA SAMWEL KAWIA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SHARTI LA KUPATIA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI (FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

## UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI

Aliyeweka sahihi hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayohusu ***"Kuchunguza Usawiri Chanya wa Mwanamke Katika Vitendawili Vya Jamii ya Wanyiha",*** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa shahada ya Uzamili ya Fasihi kwa Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……………………………………………………

Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M Sengo

(Msimamizi)

……..........................................………..

Tarehe

## HAKI MILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

# TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Mshana Samwel Kawia**, ninatamka kuthibitisha kuwa, tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, na kwamba kazi hii haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya shahada hii au tunzo yoyote.

…………………………………………

Saini

……...........................................………..

Tarehe

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa nami katika kipindi chote cha masomo yangu mpaka kufikia hatua hii ya kukamilisha utafiti huu. Napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Msimamizi wangu Prof. Dkt. Sheikh T. S. Y.M. Sengo wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kuisimamia kazi hii tangu mwanzo wa wazo. Amenijenga katika taalimu ya kifasihi kwa kunipa mawazo mengi na kuitalii tasnifu hii katika kila hatua iliyopitia. Kwa hakika usimamizi wake hauwezi kukisiwa wala kulipwa. Mwenyezi Mungu Ambariki.

Shukrani za dhati ziwaendee wazazi wangu, baba yangu Yohna Lulamso Kawia, na mama yangu, Prisca Francis Kimario, waliojitoa kwa moyo wao wa dhati wa kunilipia ada katika ngazi za Shule ya Msingi hadi Sekondari, bila kujali hali yao mbaya ya kiuchumi.

Naishukuru familia yangu, mke wangu Mageni Julius Sagenge na wanangu Brian Samwel Kawia na Braiton Samwel Kawia, ambao waliweza kuonesha moyo wa uvumilivu nikiwa katika harakati za kufanya kazi hii. Haikuwa rahisi kutimiza wajibati za kuwa mzazi na kufanya hayo mengine ya kitaalimu bila kuwapunja haki zao. Ahsanteni sana wanangu kwa kunivumilia.

Niwashukuru sana wale wote, ambao kwa namna moja au nyingine, walinisaidia katika kufanikisha kazi hii, baadhi yao walinisaidia katika ukusanyaji wa data za utafiti huu, miongoni mwao, ni Raitoni Silwimba, Newaho Mera, Agrey Nzowa. Siwezi kumsahau. Bwana Mgogo Yangson, ambaye alinisaidia kufanya tarijama ya vitendawili vilivyokusanywa kwa lugha ya Kinyiha na kuviingiza katika lugha ya Kiswahili.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke na ujumbe unaopatika katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha wanaoishi katika wilaya ya Mbozi mkoa wa Mbeya. Tasnifu hii imekusanya vitendawili kutoka katika Kata za Msia, Wasa, Igamba na Halungu, vijiji vinne vilihusishwa ambavyo ni; Igamba, Msia, Halambo na Wasa. Utafiti huu ulitumia nadharia tatu; kwanza, nadharia ya ndani-nnje ambayo ilitusaidia namna ya kuingia masikanini na kumakinika na wenyeji, kiasi cha kupunguza ugeni wa mtafiti. Nadharia hii, ilimsaidia mtafiti kupata uhusiano mzuri kati yake na watafitiwa. Pili, Nadharia ya ufeministi ilituongoza kuchunguza namna jamii ya Wanyiha inavyowasawiri wanawake katika mfumo mzima wa maisha. Tatu, Nadharia ya uhalisiya ilituongoza kuchunguza ujumbe unaopatikana katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha. Nadharia ya ufeministi na uhalisia zilikuwa mwafaka katika hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data. Mbinu tatu zilitumika katika hatua ya ukusanyaji wa data. Mbinu ya mahojiano, mbinu ya umakinifu na mbinu ya Udurusi wa nyaraka maktabani. Jumla ya vitendawaili arobaini vilikusanywa, vitendawili vitano viliteuriwa ili kutusaidia kutafuta majibu ya utafiti huu. Utafiti umepata majibu kwamba, vitendawili katika jamii hiyo humsawiri mwanamke katika hali mchanganyiko, chanya na hasi. Kwa hiyo, utafiti wetu umepata majibu kwamba, vipo vitendawili vyenye mtazamo chanya kuhusu mwanamke. Ujumbe unaopatikana katika vitendawili ni kwamba, mwanamke anapaswa kuthaminiwa sawa na mwanaume.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI** .......... **ii**
**HAKI MILIKI** .......... **iii**
**TAMKO LA MTAHINIWA** .......... **iv**
**SHUKRANI** .......... **v**
**IKISIRI** .......... **vi**
**JEDWALI** .......... **xi**
**KIELELEZO** .......... **xii**
**SURAYA KWANZA** .......... **1**
**UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Utangulizi wa Jumla .......... 1
1.2 Utangulizi wa Utafiti .......... 3
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 4
1.4 Sababu za Uteuzi wa Mada .......... 6
1.5 Tatizo la Utafiti .......... 7
1.5.1 Lengo la Utafiti .......... 7
1.5.2 Madhumuni Maalumu ya Utafiti .......... 7
1.5.3 Maswali ya Utafiti .......... 7
1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 8
1.7 Eneo la Utafiti .......... 8
1.7.1 Mipaka ya Utafiti Kijiografia .......... 8
1.7.2 Eneo la Kitaalimu .......... 8

**SURA YA PILI** .......... **9**

**UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** .......... **9**

2.1 Utangulizi .......... 9

2.2 Ufafanuzi wa Dhanna kama Zilivyotumika Katika Kazi Hii .......... 9

2.2.1 Jinsia .......... 9

2.2.2 Vitendawili (Ivhili) .......... 10

2.2.3 Usawiri .......... 12

2.2.4 Mapitio kuhusu Usawiri wa Mwanamke Katika Fasihi .......... 12

2.2.4.1 Ujumbe wa Vitendawili Katika Jamii .......... 18

2.3 Nadharia za Uhakiki .......... 20

2.3.1 Nadharia ya Ndani- Nnje .......... 21

2.3.2 Nadharia ya Ufeministi .......... 22

2.3.4 Nadharia ya Uhalisiya .......... 25

**SURA YA TATU** .......... **28**

**MBINU ZA UTAFITI** .......... **28**

3.1 Utangulizi .......... 28

3.2 Njia Zilizotumika Katika Ukusanyaji wa Data .......... 28

3.2.1 Njia ya Mahojiano .......... 29

3.2.2 Njia ya Umakinifu .......... 29

3.3 Wasaidizi wa Ukusanyaji wa Data .......... 30

3.4 Zana za Utafiti .......... 31

3.4.1 Kalamu na Karatasi .......... 31

3.4.2 Kirimbo .......... 31

3.4.3 Simu ya Mkononi (Rukono) .......... 31

3.4.4 Ngamizi ........ 32
3.5 Vyanzo vya Data ........ 32
3.5.1 Data za Msingi ........ 32
3.5.2 Data za Upili ........ 32
3.6 Uteuzi wa Walengwa ........ 33
3.6.1 Njia za Kupatia Walengwa ........ 33
3.6.2 Njia ya Uchambuzi wa Data ........ 34
3.7 Hitimishi ........ 36
**SURA YA NNE ........ 37**
**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI ........ 37**
4.1 Utangulizi ........ 37
4.2 Uwasilishaji wa Data ........ 37
4.3 Usawiri Chanya wa Mwanamke Katika Vitendawili vya Jamii ya Wanyiha 38
4.3.1 Mwanamke Anasawiriwa Kama Mama Mlezi wa Watoto Katika Jamii ........ 38
4.3.2 Mwanamke Kiumbe Mvumilivu ........ 40
4.3.3 Mwanamke Anastahiki Kupewa Hadhi Katika Jamii ........ 42
4.3.4 Mwanamke ni Kiumbe Mchapakazi Katika Jamii ........ 44
4.3.5 Ujumbe Unaopatikana Katika Vitendawili vya Wanyiha ........ 48
4.3.5.1 Mama ni Mlezi wa Watoto ........ 49
4.3.5.2 Mwanamke ni Mvumilivu Katika Jamii ........ 51
4.3.5.3 Mwanamke ni Mvumilivu kwa Mume Wake ........ 52
4.3.5.4 Uvumilivu Kipindi Cha Malezi ya Mtoto ........ 52
4.3.5.5 Mwanamke ni Mzazi Anayestahiki Kupewa Hadhi ........ 54
4.3.5.6 Mwanamke ni Mchapakazi Katika Jamii ........ 56

4.4 Hitimishi ........................................................................................ 57

**SURA YA TANO ........................................................................................ 59**

**MUHTASARI, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO .................. 59**

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 59

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti Huu ............................................. 59

5.2.1 Usawiri Chanya wa Mwanamke ..................................................... 59

5.2.2 Ujumbe Katika Vitendawili vya Jamii ya Wanyiha ........................ 60

5.3 Mambo Mapya Katika Utafiti Huu ................................................... 60

5.4 Mapendekezo ........................................................................................ 61

5.4.1 Mapendekezo kwa Wanazuoni ........................................................ 61

5.4.2 Mapendekezo kwa wanajamii ......................................................... 61

5.4.3 Mapendekezo Serikalini .................................................................. 61

**MAREJELEO ........................................................................................ 62**

**VIAMBATANISHI ........................................................................................ 67**

# JEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Uteuzi wa Wahojiwa ........................................................ 34

# KIELELEZO

Kielelezo Na. 1.1: Ofisi ya Mapokezi Kwenye Eneo la Kimondo .............................. 2

# SURAYA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi wa Jumla

Mbozi ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Mbeya. Ipo Kusini Magharibi mwa Mkoa wa Mbeya, kati ya latitudo 8$^{o}$ hadi 12$^{o}$ Kusini mwa Ikweta longitudo 12.3$^{o}$ na 33.2$^{o}$ Mashariki mwa Greenwich. Upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Ileje, Mashariki hupakana na Wilaya ya Mbeya Vijijini katika ukingo wa Mto Songwe. Upande wa Kaskazini, hupakana na Wilaya ya Chunya, upande wa Magharibi, hupakana na Wilaya ya Momba na nchi ya Zambia.

Wenyeji wa wilaya hiyo ni Wanyiha, lakini kuna jamii za wahamiaji k.v. Wandali kutoka wilaya ya Ileje, Wanyakyusa kutoka wilaya ya Rungwe na Wanyamwanga kutoka wilaya ya Momba.  Wanyiha wanaishi nyanda za juu, kati ya mita 900 – 2700 juu ya usawa wa bahari hasa katika Tarafa tatu za Vwawa, Igamba na Iyula. Ardhi ya Unyihani ni nyekundu lakini yenye rutuba inayostawisha mazao, yakiwamo ya chakula k.v mahindi, maharage, ndizi, karanga na biashara hasa kahawa. Ndani ya eneo hilo kuna kimondo chenye umaarufu mkubwa duniani kikiwa na uzito wa tani kumi na mbili. Kipo katika Kijiji cha Ndolezi, ni kivutio ambacho mpaka sasa Serikali haijafanya jitihada zozote za kuwekeza, kwani hata ofisi ya kufikia na kupumzikia wageni wafikao, hailingani na hadhi ya kimondo chenyewe.

Kimondo ambacho kilidondoka kutoka angani huko Mbozi Mbeya karibu na mji wa vwawa. Kinakadiriwa kuwa na uzito wa tani 12 na kilianguka katika mlima wa

mlenje, Kimondo hicho ni kimoja kati ya vimondo 10 vinavyojulikana duniani na kina urefu wa mita 3.3 na urefu wa mita 1.63 na kimo cha 1.22.



**Kielelezo Na. 1.1: Ofisi ya Mapokezi Kwenye Eneo la Kimondo**
Chanzo: English Version (2012)

Kwa upande wa umbile kimondo hichi kiko tofauti na vimondo vingine vinavyopatikana ulimwenguni kwa sababu kimondo hichi ni hasa kwa chuma. Chuma kimechukua asilimia 90.45 na nikel asilimia 8.69, sulfuri asilimia 0.01 na fosfori asilimia 0.11 ya masi yake. Kuna umuhimu kwa wizara husika, kuitangaza sehemu hiyo kibiashara ili kupata watalii ndani na nnje ya Tanzania. Watalii kutoka Duniani kote wanaokuja kuangalia mbuga za kusini mwa Tanzania, wataweza kwenda kuangalia hazina yetu kubwa ya tani 16 iliyoanguka katika eneo la Mbozi, miaka zaidi ya 1,000 iliyopita na kuchimbuliwa miaka ya 1930.

Jamii ya Wanyiha ni miongoni mwa jamii za kale hapa nchini, ambayo ina historia ya muda mrefu, tangu kipindi cha maisha ya utangu hadi sasa, kwa msingi huo, jamii ina mambo mengi mema ambayo ni vema yakakusanywa na kuhifadhiwa, kwa

manufaa ya wanajamii katika vizazi vingi vijavyo. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na tanzu za fasihi simulizi zilizosheheni vijitanzu kadha wa kadha vikiwemo vitendawili.

## 1.2 Utangulizi wa Utafiti

Utafiti huu ulikusudiwa kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha waishio wilaya ya Mbozi. Ili kufikia lengo lililokusudiwa, vitendawili viliainishwa na kuchambuliwa kisha kumeoneshwa mhusika mwanamke anavyosawiriwa kwa mtazamo chanya katika kazi hizo. Wanazuoni waliovutiwa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi vikiwamo vitendawili, wameonesha kwamba, mwanamke anapewa mtazamo hasi na jamii. Hali hiyo imekuwa ni chanzo cha wanawamke kuendelea kuishi maisha ya utegemezi wa kiakili na kiuchumi kutoka kwa wanaume. Usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili haujazungumzwa kwa kina cha uzamili au uzamivu. Utafiti huu umelenga kushughulikia kipengele hicho kwa upana wake.

Utafiti huu ulitumia nadharia tatu; kwanza, nadharia ya ndani-nnje ambayo ilitusaidia namna ya kuingia masikanini na kumakinika na wenyeji, kiasi cha kupunguaza ugani wa mtafiti. Nadharia ya ufeministi ilituongoza kuchunguza namna jamii ya Wanyiha inavyowasawiri wanawake katika mfumo mzima wa maisha. Tatu, Nadharia ya uhalisiya ilituongoza kuchunguza ujumbe unaopatikana katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha.

Njia tatu zilitumika katika ukusanyaji wa data; kwanza, njia ya mahojiano ilitusaidia kupata ufafanuzi wa kina kutoka kwa watafitiwa. Pili, njia ya umakinifu, ilitusaidia

kutufikisha katika uwanja wa kutegeana vitendawili, mtafiti alipata nafasi ya kujionea wenyewe, namna vitendawili vinayvotegwa, utaratibu wa kuapta majibu na ufafanuzi unaotolewa kuhusu mafundisho yaliyomo katika vitendawili. Tatu, njia ya kudurusu nyaraka maktabani zilitusaidia kupata mwelekeo sahihi wa kuandaa tasnifu hii.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Vitendawili vilianza kutumika zamani sana, tangu binadamu alipoanza kutumia lugha kama chombo kikuu cha mawasiliano. Vitendawili vililenga kupanua ujuzi wa hadhira katika elimu ya mazingira yake pamoja na kukuza wepesi wa kuwaza na kuchemsha ubongo. Vitendawili ni amali ya jamii ambayo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Sanaa hii hutegemea uwezo wa hadhira wa kutambua, kuhusisha, kulinganisha na kufumbua vilivyomo katika mazingira yanayomzunguka mwanadamu. Vitendawili hutumia wahusika wa aina mbalimbali kama ilivyo katika kazi nyingine za fasihi simulizi, kuna wahusika wanyama, binadamu, vitu na mahali. Katika utafiti huu, mhusika mwanamke ndiye aliyechunguzwa ili kuona kusawiriwa kwake.

Jamii hutumia utanzu wa vitendawili kama njia ya kumsaidia binadamu awe mdadisi katika mazingira alimozaliwa, kulelewa na kukulia. Hiyo ni miongoni mwa dhima zake katika jamii. Mfano “Ananiangalia, hali, hatembei, hacheki wala hazungumzi”. Hapo mteguaji/ hadhira lazima ifanye uchunguzi wa kina juu ya jamii yake, kitafutwe kitu kinachoweza kubeba tabia zilizotajwa katika swali la kitendawili ambalo jibu lake ni “picha”. Picha ikiwekwa ukutani, ikishikwa mkononi au kubandikwa mahali fulani, haina uwezo wa kucheka, kula wala kutembea. Kutokana

na uwezo wa vitendawili katika kufikirisha, jamii ya Wanyiha, hutumia utanzu huu ili kukuza uwezo wa udadisi kwa watoto wao. Mbali ya kukuza udadisi vitendawili vina dhima ya kuelimisha jamii kuhusu siasa, maadili na uchumi. Mfano kuna kitendawili kinachosema "*Mzungu anachungulia dirishani*", ambacho jibu lake, ni "makamasi" kinasawiri hali ya utawala wa kikoloni (wazungu). Kazi nyingi zilifanywa na Waafrika, Wazungu walikuwa wakikaa maghorofani na wakiwachungulia Waafrika. Kitendawili hicho kinaonesha hasira ya Waafrika dhidi ya utawala wa kikoloni, uliojaa dhuluma, uonevu na unyanyasaji. Waafrika waliwachukia Wazungu na kuwaona kero. Kitendawili hicho kinahamasisha Waafrika kuungana pamoja ili kupambana na utawala dhalimu.

Wahusika, katika kazi za fasihi, ni viungo muhimu sana katika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Katika utambaji wa vitendawili, wanawake ni miongoni mwa wahusika wanaotumiwa wakiwa wamebeba ujumbe mzito. Fasihi, kwa lugha ya Kiswahili, kwa jumla yake, imekuwa, ikimsawiri mwanamke katika hali ya kumdunisha kisiasa, kiuchumi na kijamii akilinganishwa na mwanamume. Senkoro (2011) anaeleza kuwa, historia ya kunyanyaswa na kugandamizwa kwa mwanamke katika jamii ni ndefu, inaturudisha nyuma kabisa wakati wa utangu, kipindi ambacho watu waligawanyika katika matabaka mbalimbali, wanaume wakipewa nafasi kubwa ya kutawala kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tangu kipindi hicho, mwanamke alilazimika kumtegemea mwanaume katika maisha yake yote na mwanaume akaanza kutumia nafasi hiyo kumnyanyasa mwanamke. Kipkorir (2004) anaeleza kuwa, unyanyasaji wa wanawake nchini Tanzania siyo jambo geni, haiwezi kupita siku

moja au mbili bila kusikia jambo linalohusiana na madhara wanayokumbana nayo wanawake.

Kuja kwa wakoloni kuliongeza unyonge wa wanawake wa Kiafrika. Liwewa (1998) anashadidiya kuwa, kuja kwa wakoloni kuliimarisha hali ya kutokuwa na usawa wa kijinsia kutokana na kuingizwa kwa elimu za kigeni. Mwanamke alitengwa asipatiwe kisomo, elimu aliyopatiwa ni ile iliyohusu mapishi, ina maana aliandaliwa kuwa mwalimu wa familiya na wa umma akiwa mama, dada, binti, nyanya, shangazi, mkwe, mamamkwe, wa shemeji. Mbughuni (1982) anasema, Dini ya Kikirstu ilimuongezea mwanamke unyonge ambapo ilimhukumu mwanamke na kumtenga kama kiumbe duni na chanzo cha maovu yote ulimwenguni. Mtazamo huu unaungwa mkono na Ade (1983) anaposema, fasihi kwa lugha ya Kiswahili, huegemea zaidi kuwapendelea wanaume, ni jambo lililorithishwa tangu kipindi cha utawala wa kikoloni ambao haukutoa nafasi ya kuwathamini na kuwaendeleza wanawake kijamii na kiuchumi. Siyo hivyo tu, bali, fasihi ya Kiafrika inampa mwanamke nafasi duni ukilinganisha na mwanaume. Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya Wanyiha.

## 1.4 Sababu za Uteuzi wa Mada

Mada hii imeteuliwa kwa sababu wanazuoni wengi Lyatu (2011), Alemu (2006), Murikarika (2011) na Kitundu (2012), waliofanya utafiti katika kuchunguza usawiri wa mwanamke katika fasihi, wamehitimisha kuwa jamii inawasawiri wanawake katika mtazamo hasi. Usawiri wa mwanamke kwa mtazamo chanya haujazungumzwa kwa upana mkubwa, jambo ambalo utafiti huu, umelipatia ufumbuzi wa kina.

## 1.5 Tatizo la Utafiti

Usawiri wa mwanamke katika fasihi umeshughulikiwa na watafiti na wahakiki kwa kipindi kirefu na kwa upana sana. Miongoni mwao ni Mbughuni (1982), Senkoro (1982 na 2011), Brigid (1994), Liwewa (1998), Lugano (1999), Alemu (2006), Ndungo (2006), Lyatuu (2011), Murikarika (2011) na Kitundu (2012) kwa kutaja wachache tu. Licha ya kutafautiana kimalengo, matokeo ya watafiti hao, yamethibitisha kuwa, fasihi kwa lugha ya Kiswahili imewasawiri wanawake katika mtazamo hasi wakilinganishwa na wanaume. Utafiti mwingi uliyotangulia, uliweka mkazo juu ya usawiri hasi wa mwanamke katika fasihi. Mwanamke ni binadamu aliyekamilika, kama alivyo mwanaume. Jee usawiri wa mwanamke ni wa aina moja katika jamii zote? Jee, ni kweli kwamba mwanamke hana mambo chanya yanayoweza kusawiriwa katika fasihi? Maswali hayo yamemshawishi mtafiti kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha.

### 1.5.1 Lengo la Utafiti

Lengo la utafiti ni kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha katika wilaya ya Mbozi mkoa wa Mbeya.

### 1.5.2 Madhumuni Maalumu ya Utafiti

(i) Kutathimini Usawiri Chanya wa Mwanamke Katika Vitendawili Vya Jamii ya Wanyiha.

(ii) Kuchunguza Ujumbe Unaopatikana Katika Vitendawili

### 1.5.3 Maswali ya Utafiti

(i) Jee ni kwa Namna Gani, Vitendawili Vya Wanyiha Huwasawiri Wanawake kwa Mtazamo Chanya?

(ii) Jee, ni Ujumbe Gani Unaopatikana Katika Vitendawili Vya Wanyiha.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Vitendawili vilikavyokusanywa vikitunzwa vizuri, wengi watapata fursa ya kuvisoma na kuvizamia mbizi, kuvifanyia utafiti zaidi na kuyatumia maarifa yaliyomo. Kwa kutumia utafiti huu, wanaharakati watatambua namna jamii ya Wanyiha inavyomtazama mwanamke tangu jadi mpaka sasa, kwani vitendawili ni sanaa kongwe. Utafiti huu umetoa picha mpya juu ya usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi, watakaosoma utafiti huu watatambua kwamba, mwanamke anao mchango mkubwa katika jamii zetu. Utafiti huu utatumika kama kitambulishi cha Wanyiha katika jamii kubwa ya Tanzania.

### 1.7 Eneo la Utafiti

#### 1.7.1 Mipaka ya Utafiti Kijiografia

Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Mbeya, wilaya ya Mbozi, katika jamii ya Wanyiha tu. Vijiiji vinne; Halambo, Msiya, Igamba na Wasa vilihusishwa. Eneo hilo liliteuliwa kwa sababu idadi kubwa ya wakaazi wake wa asili, ni Wanyiha, ambao ndiwo walengwa wa kazi hii.

#### 1.7.2 Eneo la Kitaalimu

Katika utafiti huu, uchunguzi ulijikita katika kijitanzu cha vitendawili peke yake. Usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya Wanyiha umeshughulikiwa pia uchunguzi ulifanyika kuhusu ujumbe unaojitokeza katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha vile vyenye usawiri chanya kwa mwanamke.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Utalii unaotajwa hapa ni ule wa kusoma marejeleo kwa kina ili kupata mawazo ya wanazuoni waliotangulia, kuandika makala, vitabu na tasnifu. Ni muhimu kutalii kazi zao ili kuongeza ujuzi, ubora na maarifa katika kazi yetu. Kumar (2011) anasisitiza kwamba, ipo haja kubwa ya kutalii kazi za wanazuoni waliotangulia, kwa sababu ya kupatikana nafasi ya kutambua vipengele vilivyochunguzwa na ambavyo bado. Kwa kufanya hivyo, ni rahisi kupata mapengo ya utafiti ambayo yanapaswa kuzibwa kitaalimu.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhanna kama Zilivyotumika Katika Kazi Hii

### 2.2.1 Jinsia

Jinsia ni kipimo kinachotumika kupima hadhi ya mtu katika jamii. Ni tafauti na jinsi, ambayo ni istilahi ya kibailojia zaidi. Jinsia inahusu mtazamo wa jamii, wanadamu wanavyopeana wajibu kulingana na tafauti zao za kijinsi. Mfano wanawake wamekuwa wakipewa hadhi duni na wanajamii ikilinganishwa na wanaume, wengi wao wanaendelea kuamini kuwa, mwanamke hawezi kujitegemea mwenyewe bila ya mwanaume. Jambo hilo linapewa nguvu zaidi na Ripoti ya Umoja wa Kimataifa (1980) inabainisha kuwa, wanawake idadi yao ni kubwa zaidi kuliko wanaume, hufanya kazi zaidi ya theluthi mbili ya kazi zote. Kutokana na kazi wanazozifanya mapato yao ni asilimia kumi ya mapato yote, wanawake humiliki asilimia moja ya mali zote duniani. Kwa kawaida tamaduni za Kiafrika hufanya upendeleo kwa wanaume dhidi ya wanawake. Wanaume ndiyo wenye haki ya kupewa urithi wa

mashamba, nyumba, ardhi na hata kushika nafasi za juu katika uongozi (women Affairs and Children (1995).


Katika jamii ya Wanyiha tabia ya kuwapendelea wanaume ipo kwa kiasi kikubwa. Kiuchumi, ni kwamba mwanaume ndiye mmiliki mkuu wa mali yote inayozalishwa katika familia, bila kujali ushiriki na mchango wake katika uzalishaji mali. Mwanaume hupewa nafasi ya kufanya maamuzi yote juu ya familia, mwanamke hutoa maoni na ushauri nnje ya vikao. Katika mazingira mengine, mama hulazimika kuandaa chakula kizuri, chenye virutubishi kwa ajili ya mume wake hasa nyama (*ishundu*) iliyoanikwa darini (*pigulu*) kwa muda wa wiki hadi miezi kadhaa, aghalabu mtoto hawezi kupewa wala mama. Jambo hilo linatajwa pia katika jamii ya Vasu, Nicholaus (2011) *Nyama yedi ni ya mume (*nyama nzuri ni ya mwanamume) hata hivyo anaeleza kuwa, athari ya tabia hiyo, ni akina mama na watoto kuendelea kusumbuliwa na tatizo la utapia mlo.

### 2.2.2 Vitendawili (Ivhili)

Vitendawili katika lugha ya Kinyiha huitwa *Ivhili Ivyakusumba* ni aina ya mafumbo yanayohitaji jibu la haraka, mafumbo hayo huwa na mianzo na miishio maalumu. Ni semi fupifupi zinazofumbwa na hutolewa kwa hadhira ili ziweze kufumbuliwa, ni kauli za kutegwa zinazohitaji kuteguliwa. Ufumbuzi wake hutegemea uwezo wa hadhira kutambua vyema mazingira yao kwa kulinganisha swali la kitendawili na vitu vinavyowazunguka, hivyo jibu linalotolewa lazima lisadifu mazingira ambamo kitendawili kilitegwa. Aidha, vitendawili hutumuia tamathali na ishara kuelezea jambo lililofichika ambalo ndilo jibu la fumbo. Jibu linaweza kuwa ni neno moja au kifungu cha maelezo, lakini ufafanuzi lazima utolewe ili kupata uhusiano uliopo kati

ya swali (fumbo) na jibu lake. Mfano “Ameingia shimoni akiwa uchi, *akatoka amevaa nguo nzuri”*. Jibu, mbegu ya hindi, hupandwa ikiwa tupu (uchi) lakini wakati wa kuvunwa, mbegu ya hindi huzungukwa na majani ambayo hufananishwa na nguwo.

Uwezekano wa kuteguliwa kwa kitendawili, hutegemea mambo matatu; kwanza, mazingira ya jamii, pili, historia ya jamii, tatu uhalisiya wa jambo. Hii ina maana kwamba, kitendawili kimoja, kinaweza kuwa na maana nyingi katika jamii tafauti tafauti. Pia katika jamii moja, kitendawili cha aina moja, kinaweza kuwa na maana tafauti tafauti kutegemeana na vipindi vya ujuzi na teknolojia ya jamii, mfano.




(a)

(b)

(c)

Majibu yote matatu ni sahihi. Jibu la kwanza, *binadamu na kivuli chake* lilikuwa mwafaka katika kipindi cha utangu, kipindi ambacho binadamu alikuwa bado hajaweza kutengeneza kitu kinachosawiri swali la kitendawili. Katika uhalisiya, binadamu anapotembeya, kivuli chake, huwa nyuma yake au mbele yake, lakini binadamu hawezi kuongeza au kupunguza mwendo ili aende sambamba na kivuli hicho. Jibu la pili, *tairi za baiskeri* ni jibu lililopatikana baada ya binadamu kuanza

kutumia baiskeri kama nyenzo ya usafiri, tairi ya mbele na ile ya nyuma daima haziwezi kukamatana, kila moja hutembea kwa kasi yake bila kuingiliana. Jibu la tatu, *tairi za gari*, jibu hilo lilianza kutumika baada ya jamii kupata maendeleo ya ubunifu wa kutengeneza gari kama nyenzo ya usafiri, hata hivyo, tairi nne za gari haziwezi kukutana pamoja ijapokuwa muda wote zinakimbia zinapokuwa barabarani.

### 2.2.3 Usawiri

Usawiri ni istilahi katika taalimu ya kifasihi, yenye maana ya taswira za wahusika wa fasihi zinazoundwa na wasanii ili kuwasilisha tabiya na matendo mbalimbali ya binadamu katika maisha ya halisi. Istilahi hiyo imekuwa ikitumiwa zaidi na wahakiki wanapochambua kazi za fasihi hasa katika kipengele cha wahusika. Katika mazingira hayo, wahakiki huonesha mitazamo na fikra zao kulingana na jinsi walivyozielewa kazi za wasanii. Kwa hiyo usawiri chanya, ni taswira sahihi na halisi wanazostahili kupewa wahusika katika kazi za fasihi.

### 2.2.4 Mapitio kuhusu Usawiri wa Mwanamke Katika Fasihi

Mwanamke hupewa nafasi hizi na zile, duni akilinganishwa na mwanaume. Mtafiti akiwa masikanini alipata maelezo yafuatayo kuhusu usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wanyiha, Mwashilindi (2014).

> *''Kufuma uluvhalilo lwahali, avhatata vhatahavhapanga avhamayi uvhuzila navhumo uwakuyanga na kuvhapanzya nashimo. Tungati vhatahavhapangamalaga poshe ingevhali ni nsivho inyinza zihasyalaga mwe-mmwoyo''*. lakini ilelo ili, vhakwimila pa – vhanavuli, nukukuyanga amazwi gegalipo. Mmmmm! Serikali yavhapoha!
> Tangu kale babu zetu hawakuwajali wanawake wala hawakupewa nafasi yeyote ya kutoa mchango wa mawazo hata katika mambo yaliyowahusu wao. Mawazo mazuri waliokuwa nayo, yalibaki kuwa hazina yenye machungu katika nafsi zao. Lakini leo hii, wanasimama mbele ya wanaume na kutoa

> mchango wa mawazo katika mada inayojadiliwa. Mmmm! Serikali imewaokoa (Tarjama ya Mgogo, Y).

Kazi zilizofanywa na Ade (1983), Kipkorin (2004), Chaliga (2011), Kitundu (2012), Mbiu (2013), zimethibitisha kuwa, kuna mtazamo hasi wa kijamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Utafiti huu ulikusudia kuitazama jamii ya Wanyiha kwa jicho kali zaidi, kupitia katika kijitanzu kikongwe cha vitendawili, ambacho kipo tangu kipindi cha utangu hadi leo hii, tumepata kuelewa kuhusu nafasi ya mwanamke wa Kinyiha tangu enzi za jadi. Hata hivyo, fasihi ya Wanyiha haikuwasawiri wanawake katika mtazamo huo hasi pekee yake, bali ilimtazama mwanamke katika uhalisiya na kuthamini mchango wake chanya kama data za utafiti zilivyoonesha katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za kazi hii.

Mdee na Mbogo (1985) wanaeleza kuwa, uwanja wa uhakiki na uchambuzi wa wanazuoni wa vitendawili, hususani, vile vya Kiswahili, na vya Afrika kwa jumla ni mchanga mno. Inawezekana sababu moja kubwa ya hali hii ni kuwa vitendawili vinahusu watoto zaidi, navyo vimejikita katika kuwachangamsha na kuwaburudisha watoto baada ya kazi, wakati wa usiku. Mtafiti anaona kuwa, ipo haja ya kufanya uchunguzi wa kina juu ya vitendawili ili kuibua mambo mengi yenye manufaa zaidi badala ya kuendeleza hoja ya kwamba, hicho ni kijitanzu cha watoto chenye lengo la kuburudisha na kuwachangamsha watoto tu. Vitendawili ni mafumbo, fumbo hufumbiwa mjinga, mwerevu hulifumbuwa, huanza na elimu ya mazingira hadi kwenye mafumbo makubwa (elimu ya falsafa).

Matteru (1982) alichunguza kazi za fasihi ya Kiswahili, anaainisha picha tatu za mwanamke katika fasihi, kwanza, mwanamke kama mzazi, kazi yake ni kuzaa na

kulea watoto. Pili, mwanamke kama chombo cha anasa ya mwanaume kazi yake ni kuburudisha nafsi yake na ile ya mwanaume. Tatu, mwanamke ana haki ya kupendelewa na kutegemewa, kazi yake ni kutumika kama chombo cha kuzalishia mali kwa ajili ya familiya yake. Mbughuni (1985) alichunguza kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili, anaainisha picha mbili za mwanamke. Kwanza, ni kiumbe mharibifu, pili ni kiumbe mwongofu. Wahakiki hao wamejikita kuonesha uovu wa mwanamke katika jamii. Sengo (2014 darasani) anasema, kwa Waislamu, mwanamke ni bustani, kipumnzishi cha nafsi za mke na mume na aliumbwa kwa makusudi hayo.

Mwanamke asiyekubali hali hiyo, anamkana Mwenyezi Mungu. Mtafiti anaona kwamba, uongofu na uharibifu unaotajwa na Mbughuni ni jambo ambalo linaweza kujitokeza hata kwa wanaume, jee mara ngapi tumeshuhudia uharibifu wa wanaume? Jee wafungwa magerezani ni wanawake watupu? Ni vema suala la usawiri wa wahusika lizingatie uhalisiya wa jambo na siyo hali ya kutumia mazoeya yaliyoelezwa na Mbiu (ktj), Chaliga (ktj), Kitundu (ktj), Kipkorin (ktj), Ade (ktj) wanazuoni waliotutangulia. Ni wajibu wa watafiti wa leo, kufanya kazi zao kwa kutumia nadharia zinazoleta picha halisi za mambo yaliyomo kwenye jamii zetu.

Ndungo (2006) alifanya utafiti wa usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wakikuyu kwa kutumia fasihi, lengo lilikuwa ni kuona mtazamo wa jamii kuhusu mwanamke. Utafiti ulibaini kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe duni, anayeishi kwa kutegemea akili na uwezo wa mwanaume, k.v kuchaguliwa wachumba kwa kuzingatia uzoefu wa maisha, kunyimwa nafasi za uongozi, kutoshirikishwa katika maamuzi ya kijamii, kunyimwa urithi wa mali. Majibu ya utafiti wa Ndungo yameonesha usawiri hasi wa mwanamke wa Wakikuyu, utafiti huu, umetupatia

majibu tafauti, umeonesha kuwa mwanamke katika jamii akitumiwa kwa kuzingatia uhalisiya wake, ana mchango chanya, ni mlezi, mshauri na mchapakazi wa familia. Jambo la msingi ni kupewa nafasi ya ushiriki wa mambo hayo. Mfumo wa haya kutafautiana kutoka jamii hadi nyingine.

Chesaina (1991) alifanya uchunguzi wa taswira ya mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Kalenjini nchini Kenya, Utafiti ulibani kuwa, wanawake wanafananishwa na watoto wadogo, wanahitaji kulindwa na kuongozwa na wanaume. Si ila, bali ni tunu waliyopewa kimaumbile. Mtazamo huo upo tangu kale, jamii nzima inaamini na inatambua hali hiyo. Wanawake wenye kupinga utamaduni huo ni wenye kuathirika na utamaduni wa Kimagharibi. Kipury (1983 na 1989) anashadidiya kuwa unyonge wa mwanamke katika jamii ya Wamasai ni jambo ambalo lipo tangu kuumbwa kwa ulimwengu huu, ndiyo maana hata kazi wanazopewa ni zile ndogo ndogo k.v kupika, kuokota kuni, kuchota maji, kuosha vyombo na kukamua maziwa. Upungufu wa nguvu kwa mwanamke, kisitumike kama kigezo pekee cha kumlinganisha na mtoto, vitumike vigezo vyenye mashiko kama fikra, utashi, hekima n.k. Mwanamke wa Kiafrika amepewa vyeo tisa, ambavyo kila kimoja, ni ishara ya heshima na hadhi kwake. Sengo (2014 darasani) anavitaja kwa majina.

1. Anaitwa mama na watoto aliowazaa.
2. Anaitwa dada na ndugu aliozawa nao.
3. Anaitwa nyanya na wajukuu wa kizazi chake.
4. Anaitwa mke na mume aliyemuoa.
5. Anaitwa mkwe. Mke wa mjomba kwa watoto wa wifi zake

6. Anaitwa mama mkwe na;

   (i) Waume wa mabinti zake

   (ii) Wake wa vijana wake

   (iii) wazazi wa Mume wake

7. Anaitwa shangazi na watoto wa kaka zake.

8. Anaitwa shemeji na wakubwa au ndugu wa mumewe.

9. Anaitwa binti kwa baba zake.

Wanafasihi wa Kiafrika wanalipa uzito jambo hilo na kulichambua kulingana na mazingira. Wanawapa thamani kubwa akina mama. Waswahili wana maneno yao yanayoonesha umuhimu wa mama katika jamii. Wanafasihi wanabeba wajibu wao wa kuelezea hali hiyo kwa njia ya kisanii, wao hutumia maneno machache k.v, "Nani kama mama!" Hakuna mzazi na mlezi amshindaye mama. Mama kwa mwanawe. Pia kuna vitendawili kama; Mama hachoki kunibeba (kitanda). Mama hatui mzigo wake (konokono). Mzigo mzito unapomshinda kuubeba kichwani (kama baba au jamii) huangukia fuzini. Mama hubeba mzigo wote juu ya mtoto. Hupata taabu za kujifunga, kujifungua na kulea. Uchungu hasa wa uzazi aujua mama, baba ni mhudumu tu.

Fasihi ikitumika vibaya inaweza kuwa ni nyenzo ya ukandamizaji wa wanawake. Alemu (2006) alifanya utafiti juu ya usawiri wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Oromo waishio eneo la Jimma katika nchi ya Ethiopia. Lengo la utafiti lilikuwa ni kuchunguza namna fasihi simulizi inavyotumika kama silaha ya ukandamizaji dhidi ya mwanamke. Utafiti ulibaini kuwa, mwanamke anagandamizwa kutokana na misingi ya utamaduni ambayo chimbuko lake ni miiko,

imani na mazoea ya kijamii ambayo humpendelea mwanaume na kumbagua mwanamke, kumshirikisha katika maamuzi juu ya maisha yake. Maelezo hayo yameonesha kuwa, tanzu za fasihi simulizi vitendawili, hadithi, methali na nyimbo hutumika kuhalalisha unyonge wa mwanamke. Hata hivyo, kazi ya fasihi siyo kuonesha maovu yaliyomo katika jamii, bali ni nyenzo ya kufichua yaliyomo kwenye jamii. Utafiti huu umetoa mtazamo chanya ambao ni tafauti na namna Alemu alivyoeleza juu ya mwanamke.

Wapo wanafasihi wanaoafiki kuwa, mwanamke anapaswa kusawiriwa katika uhalisiya wake ili kuonesha mchango wake halisi katika jamii. Momanyi (2007) anasema wanafasihi hawana budi kufikiria upya namna ya kuunda mhusika mwanawake, wamsawiri kulingana na yale anayoweza kufanya bali siyo yale anayofikiriwa kuwa anaweza kufanya. Mwanamke anaweza kujisimamia mwenyewe katika kijiletea maendeleo kama ilivyo kwa mwanaume, usawiri wa aina hiyo ukizingatiwa, utampatia mwanamke nafasi inayostahili katika nyaraka za kihistoria.

Jambo linalosisitizwa hapo ni kwamba, wasanii watumie sanaa zao, kuwanasua wanawake katika wimbi zito lililojaa ulitima na utule, wimbi linalogubika vipawa vyao, mwanamke asawiriwe katika misingi ya kiuhalisiya na siyo katika misingi ya kimazoea. Katika utafiti huu, uchunguzi umefanyika kwa kutumia nadharia ya uhalisiya, hivyo majibu ya utafiti huu, ni maelezo halisi juu ya wanawake wa jamii ya Wanyiha.

Utafiti mwingine unaoshabihiana na huu wetu ni wa Sengo (1985) ambapo mtafiti alichunguza utendaji wa hadithi (ngano) za Unguja. Ingawa lengo lake halikuwa

kuchunguza usawiri wa mwanamke, lakini miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na mtafiti ni suala la hadhi na nafasi ya mwanamke katika ngano. Katika matokeo yake ameeleza kuwa, baadhi ya hadithi hizo, zinamsawiri mwanamke kama kiumbe duni. Kutokana na maoni yake Sengo (ktj) anasema uduni wa mwanamke unaosawiriwa katika ngano za Unguja, hugusa wanawake wote wa Afrika. Utafiti wa Sengo umetupatia mwanga kuhusu masuala yanayohusu wanawake, tunafikiri kuwa utafiti huu ni mwafaka kwa kuwa umejikita katika kijitanzu cha vitendawili ambacho ni tafauti na kile cha ngano kilichoshughulikiwa na Sengo, isitoshe kuna uwezekana kwamba, kazi ya Sengo ilisawiri hali halisi ya maisha ya jamii ya Pwani ambayo huenda imeathiriwa na tamaduni za wageni wa Mashariki ya mbali na kati ambao wameishi huko kwa karne nyingi. Pengine hali hiyo inaweza kuwa ni tafauti na jamii ya Wanyiha, kama asemavyo Sengo (2009) kuwa fasihi ina kwao. Wanyiha kwao ni nyanda za juu Kusini Magharibi katika nchi ya Tanzania, ni jamii hai, iliyojengwa na ya kwao ambayo utafiti huu umetujuza.

#### 2.2.4.1 Ujumbe wa Vitendawili Katika Jamii

Ujumbe wa vitendawili, ni mafundisho yote yanayopatikana katika kazi za fasihi. Vitendawili, huhamasisha utendaji wa kazi kwa vijana. Katika mahojiano kati ya mtafiti na Nzowa (2014), tulibaini kwamba, katika jamii ya Wanyiha babu na bibi, waliandaa baadhi ya shughuli zilizofanyika muda ambao walikuwa wanaendelea na usimuliaji wa hadithi, shughuli hizo ni kama vile, kumenya karanga, kupukuchua mahindi, kumenya maharage, kusokota kamba za kufungia mifugo kwa wavulana. Katika mazingira hayo, kazi kubwa zilifanyika bila kuchoka kwa sababu wakati kazi zinaendelea, vitendawili viliwaburudisha na kuwafanya wasione ugumu wa kazi zao

na walizifanya kwa muda wa masaa mengi. Kwa upande mwingine wazee walipata nafasi ya kuchunguza kwa karibu zaidi namna vijana wao wanavyoweza kujituma katika kazi, vijana wavivu walielekezwa athari za tabia hizo na wachapakazi walipewa kongole au pongezi kwa jitihada zao. Kutokana na maelezo hayo, mtafiti anaona kwamba, vitendawili Unyihani vilitumika kama sehemu ya kupatia taalimu kwa vijana, kwa wakati mmoja, vijana walipata mafundisho kuhusu maadili mema na uwajibikaji wa kazi za mikono.

Vitendawili ni nyenzo ya kusambazia itikadi za jamii. Mbughuni (1983), TUKI (1985) na Mulokozi (1989) wanaeleza kuwa, mbali na kufundisha na kufikirisha, vitendawili kama ilivyo katika vijitanzu vingine vya fasihi simulizi, hubeba itikadi fulani kwa ajili ya kuihifadhi na kuisambaza kwa wanajamii. Itikadi hiyo inaweza kuwa ya kijumuia, kitabaka au kijinsia. Mafundisho katika vitendawili hayawalengi watoto tu, bali jamii nzima. Wazo hilo linaungwa mkono na Japhet (1977) anayesisitiza kuwa wazee ndiyo mabingwa wa vitendawili. Maelezo hayo yalitusaidia kuzama zaidi ili kupata mambo mazito yaliyojificha katika vitendawili vya Wanyiha, dhima za vitendawili vilivyokusanywa na mtafiti, zimewekwa wazi katika utafiti huu.

Finnegan (1976) anashadidiya kuwa, dhima ya kuburudisha katika vitendawili inapewa nafasi ya kwanza, mara kwa mara huwa inafungamana na nyingine kama kukosoa, kutunza mila na dasturi za jamii, kuelimisha na kuadilisha. Finnegan (ktj) anasema, kuelimisha ni dhima ya pili kwa uzito, kutokana na upana wa maudhui yake, lakini hasa, dhima yake kuu ni kuburudisha. Mtafiti ameona kuwa, dhima ya kuelimisha na kuburudisha, zote zina uzito sawa, katika muktadha wa kifasihi, kwa

sababu kila moja huundwa kwa madhumuni ya kipengele maalumu kinachojipambanua katika fasihi. Dhanna ya kuburudisha ni matokeo ya vipengele vya fani ambavyo ndani yake kuna sanaa nzito katika uundaji wa wahusika, matumizi ya lugha n.k na kuelimisha ni matokeo ya vipengele vya maudhui, vipengele hivyo viwili, hutegemeana na kukamilishana kifasihi. Hata hivyo, katika utafiti huu, dhima ya kuburudisha haijashughulikiwa kikamilifu, kwani hayakuwa madhumuni ya utafiti huu.

Mtafiti ameona kuwa, ujumbe uliomo katika vitendawili ni kujenga umoja na ushirikiano miongoni mwa vijana. Vitendawili vilisaidia kuwakusanya vijana wa maeneo tafauti katika eneo moja; katika mazingira hayo, walipata nafasi ya kufahamiana na hatimaye kujenga urafiki na udugu miongoni mwao. Jambo hilo lilipata nguvu zaidi wakati wa kutegeana vitendawili kwa njia ya ushindani wa vikundi, kila kundi hujipanga na kuandaa vitendawili vinavyopaswa kuteguliwa na kundi jingine, vijana huendelea kupendana na kuheshimiana kulingana na mchango wa kila mmoja katika kikundi chake.

## 2.3 Nadharia za Uhakiki

Neno nadharia, kama dhanna katika, kazi za fasihi limefananuliwa na wanazuoni wengi. Baadhi yao ni Sengo (2009) Carter (2006), Ntarangwi (2004), Owhida (2006), Njogu (2007) kwa pamoja wanakubaliana kwamba nadharia ni miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi, kuifahamu kazi hiyo katika vipengele vyake vyote. Mushengyezi (2003), zipo nadharia nyingi ambazo hutumika, kuchunguza na kuhakiki kazi za fasihi, kutokana na mabadiliko yanayotokea kila siku; Nadharia nazo huendelea kuibuka, mpya huzuka na za zamani, kutazamwa kwa

jicho kali zaidi. Mfano nadharia nyingi za Umaksi na Ukomunisti, Ubepari na za Kikoloni, hazipawi nafasi kubwa sana hapa nchini Tanzania na hasa kwa wanafunzi wa Sengo, anayesisitiza kwamba, dunia yote ni ya binadamu wote na wana yao huko waliko. Hali hii inatokana na ukweli kwamba katika fasihi na ulimbe wa jamii, hakuna kilicho sahihi, dumu dumifu, kilichokuwa sahihi jana, kesho kinaweza kuwa siyo sahihi. Hakuna nadharia bora zaidi ya nyingine, nadharia zote zina ubora wake kulingana na kazi, pahala na wakati.

### 2.3.1 Nadharia ya Ndani- Nnje

Nadharia ya ndani-nnje, Sengo (1985 na 2009), inasema kwamba, ili kujua utamaduni wa jamii ya watu ni lazima kwanza mtu atambue fikra zao, mtazamo na mawazo yao. Sengo (2009) anasisitiza kuwa, mtafiti, mwalimu au mhakiki wa fasihi ya jamii fulani, ili aweze kuitafiti, kuifundisha au kuihakiki jamii, shuruti aimanye vizuri. Kuijua fasihi ya watu ni muhimu, kwanza, kuwajua binadamu wenyewe, utamaduni wao, mila zao, ada na dasturi zao, ambazo ni ishara na dhanna zao. Msingi wa nadharia hii, ni kwamba, katika kazi ya utafiti ni lazima pawapo na uhusiano wa karibu kati ya mtafiti na watafitiwa.

Ndani ni ndani. Ndimo mlimo kokwa za chungwa, embe, zaituni. Nnje ni huko kwenye ganda, kunakoshikwa. Mwona nnje, hakika, hajaona ndani. Mambo ya jamii, sharti yazingatiye kweli za ndani. Ili kujua ubinadamu, tabia au undani wa binadamu, sharti kujua maisha yake tangu utotoni, mazingira aliyokulia na kulelewa, kisha kujenga naye, mazoweya ya muda mrefu. Kwa kufanya hivyo, yatapatikana mazuri na mabaya yake yote yaliyojificha. Bila kufanya hivyo, mtafiti atajikuta amepata data nyingi zisizokuwa makini na kupata majibu yasiyoweza kutatua tatizo la utafiti.

Ubora wa nadharia hii ni kwamba utafiti ni kazi ya kitaalimu inayohitaji uchunguzi makini tena wa muda mrefu wenye kuhusisha weledi, udadisi na uchambuzi wa kina.

Mambo hayo yanahitaji mazingira mazuri ya uhusiano baina ya mtafiti na watafitiwa, jambo hili haliwezi kukamilika kwa muda wa siku, wiki, wala mwezi mmoja bali linahitaji miezi ya kutosha hadi miaka kadhaa. Nadharia hii itatumka katika kazi hii kwa sababu mtafiti anategemea kupata ushirikiano wa karibu sana kutoka kwa wasaidizi watakaopatikana katika mazingira ya utafiti. Nadharia ya Ndani - Nnje imejikita zaidi na jinsi ya kuingia masikanini na kumakinika na wenyeji, kiasi cha kupunguza ugeni. Isitoshe, data zinazokusanywa, zina vipengele vya fani na maudhui, ili mtafiti aweze kuvifafanua vipengele hivyo, sharti ajue undani wake kama nadharia inavyotuongoza.

### 2.3.2 Nadharia ya Ufeministi

Wollstonecraft (1792), anatajwa kuwa ni miongoni mwa waasisi wa nadharia ya Ufeminist, anasema kuwa mielekeo hasi kumhusu mwanamke imesababishwa na elimu mbovu wanayopewa wanawake na wanaume. Beauvoir (1952) aliunga mkono kwa kusema kuwa asasi za dini, ndowa na utamaduni zinamdunisha mwanamke. Dini humkandamiza mwanamke kwa kutaka awe mnyenyekevu, ndowa inasisitiza uwezo mkubwa wa mwanaume dhidi ya mwanamke, utamaduni humsawiri mwanamke kama kiumbe duni mbele ya mwanaume. Sengo (2014) darasani, anatafautiana kimtazamo na maelezo hayo, Dini ya kweli ni ya Muumba Mmoja, Mungu Mmoja wa kweli! nani wa kumpinga? Kwa mantiki hiyo, hakubali kwamba dini humkandamiza mwanamke, bali Dini haibagui mwanamke wala mwanaume,

wote wana haki sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kila mmoja, kwa maumbile yake, kapangiwa yake.

Ufeministi una mizizi katika siasa za ukombozi wa wanawake. Harakati hizo zilianza miaka ya 1960 huko Marekani. Moja ya mambo yanayozingatiwa ni kuunda upya uhalisiya wa mwanamke kwa kupangua na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanaume na kumkandamiza mwanamke. Hizo ndizo fikira zilizoenea Ulaya na Marekani. Katika kutekeleza harakati hizo nyanja tatu zimepewa msisitizo Kwanza, ni ufeministi huru, ambao unayatazama maisha ya jamii na uamuzi wa kupata watoto, uwe wa wote wawili, yaani mwanamume na mwanamke. Akipatikana mtoto, malezi yasiwe ya mwanamke, iwe kazi ya malipo kama kazi nyingine. Kwa Wanyiha, mawazo haya hayaingii akilini kwa sasa. Pili, ufeministi wa kijamii, unasisisitiza kwamba hali ya maisha ya mwanadamu ni zao la uhusiano wa kijamii ambao huendelezwa na kubadilishwa na jamii inayohusika. Mfumo huu hauchukulii mfumo wa kuumeni kama dhanna ya muundo wa ukandamizaji. Kwa mtazamo huu, wanaume wanapaswa kuhusishwa katika kulea watoto na kuwaacha wanawake wafanye uchaguzi wa maisha yao. Nalo hili ni geni mno kwa Wanyiha. Wanyiha na Watanzania wana taratibu za kulifanya hilo lisemwalo. Si lazima waige ya kigeni. Tatu, ufeministi mkali ni wa kundi linaloona kuwa mwanamke hana nafasi ya kuwa huru katika jamii kutokana na kukandamizwa na mwanaume.

Kutokana na tafauti ya maumbile, suluhu ni kutenganisha wanawake na wanaume ili wanawake waweze kutawala miili yao na maisha yao bila kuongozwa na wanaume. Ni jambo gumu kumtenganisha mwanaume na mwanamke kimaisha kwa kumtaka kila mmoja awe na maisha yake, kwani viumbe hawa wawili lazima waishi pamoja

ili kuendeleza vizazi na malezi kwa watoto. Si jambo la kuchagua. Muumba (akubalike asikubalike) kaumba Mbingu na Ardhi kama zilivyo, kaumba vingine vyote, kama vilivyo. Hakuna wa kuyabadili maumbile hayo.

Kazi za akina Shwalte (1977), Gilbert na Gubar (1979) na Jacobs (1979) zinafafanua na kuunga mkono nadharia za ufeministi mkali, ufeministi wa kijamii na ufeministi huru. Ufeministi katika nchi za Kimagharibi unatupatia tafsiri kuwa, wanaume walisawiriwa kama madui wanaostahili kupigwa vita na wanawake. Ukweli ni kwamba, ufeministi umesaidia kudhihirisha kwamba, wanadamu wamelelewa ili kuchukua nafasi maalumu za kijamii zenye kuonesha uhusiano kati ya mwanawake na mwanaume. Wafeministi wanaona kuwa uhusiano wa jadi kati ya mwanaume na mwanamke uangaliwe upya ili kuwapa wanawake na wanaume nafasi sawa. Ufeministi unasisitiza pasiwapo masharti ya kuchagua jambo kwa misingi ya jinsia. Maumbile nayo yana nafasi yake katika kulitekeleza hilo lisemwalo kwani, wazee wa Kizaramu, walikwisha lisemeya, "zilongwambali, zitendwambali", linalosemwa ni moja, linalotendwa ni la pili.

Wanafasihi wa Kiafrika wanamtazamo wao juu ya nadharia ya ufeministi katika kuhakiki kazi za fasihi. Ntarangwi (2004) anasema kwamba, mhakiki anayezingatia nadharia hii, huitazama kazi ya fasihi kuwa, imeundwa kutokana na misingi ya kijinsia inayosukumwa na nguvu za mtunzi. Mtunzi huwasawiri wahusika wake kulingana na mtazamo wa jamii yake, mara nyingi maoni ya mtunzi hutokana na fikra zake binafsi au mafundisho aliyoyapata ndani ya jamii yake iliyomlea na kumkuza. Kinachozungumzwa hapa ni kwamba, wahakiki na watafiti wa kazi za fasihi, wanapoitumia nadharia ya ufeministi, uchambuzi wao uzingatie matakwa,

mielekeo na utamaduni wa jamii husika, kwa sababu kila jamii ina mambo yake, maisha ya Ulaya au Marekani siyo sawa na maisha ya Waafrika wala maisha ya Wazaro, Wachaga siyo sawa na maisha ya Wanyiha. Kwa kuwa lengo la utafiti ni kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha, nadharia hii ilituongoza vema kuonesha nafasi wanayopewa wanawake wa Kinyiha tangu jadi mpaka sasa. Nadharia hiyo ilikuwa mwafaka kujibu swali lililouliza, Jee, ni kwa namna gani, jamii ya Wanyiha huwasawiri wanawake kupitia katika vitendawili?

### 2.3.4 Nadharia ya Uhalisiya

Sengo (2009), anasema, nadharia ya uhalisiya ni hali halisi ya pahala fulani au jambo fulani. Penye ukame huzungumzwa njaa, kutopatikana kwa maji na taabu za kukosa vitu fulani fulani. Uhalisiya wa kimiktadha na mandhari ya kazi za fasihi, imejikita katika kweli zote ziihusuzo hali hiyo. Mtunzi au mwandishi alivyo, alikozawa, alikolelelwa, alikosomeshwa na uwakala aliorudi nao, au na uzalendo alo nao. Uhalisiya ni nadharia pana na kubwa, isipelekwe Ulaya wala Marekani, Uhalisiya usomwe viamboni, vijijini, mitaani, na nadharia itumike kwa upana wake.

Sengo anaona kwamba, katika jamii yake, mambo yote yanayofanyika yanapaswa kujikita katika mazingira halisi. Baadhi ya vipengele vinavyofanyiwa hujuma na kupoteza uhalisiya wake katika maisha ya wanazuoni, ni kuficha kazi mbalimbali za waandishi wa vitabu. Wapo baadhi ya watu, huthubutu kufuta majina ya waandishi halisi na kuandika majina yao ili zionekane kazi hizo ni zao. Huo siyo uhalisiya, ni uonevu na jeuri. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004) nadharia ya uhalisiya katika upana wake, ni ya uwakilishi wa ukweli wa mambo katika maisha. Mhalisia husadiki

matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa katika tajiriba ya maisha. Hivyo uhalisiya wa Kiafrika, hujikita katika mambo yaliyopo, matukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuonekana. Kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Hivyo, picha za ulimwengu atakazounda msanii, zapaswa kudhihirisha hali hiyo.

Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisiya, hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisiya wa mambo kupitia kwa wahusika aliowasawiri. Mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo ya wakati maalumu. Kwa muhtasari, msanii anatarajiwa, kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati huo. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kiuhalisiya. Watu wa Ulaya huko Ufaransa Emmanuel Kant, Schiller, Flaubert wanaihusisha dhanna ya uhalisiya na mambo mawili. Kwanza, inatumika kama njia ya kutathimini ukweli wa maisha.

Pili, hutumiwa katika uhalisiya wa kifasihi unaoashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Hiyo fasili ya pili, ndiyo iliyotumika huko Ufaransa katika mwaka 1850 kuelezea kazi ya sanaa iliyoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyokuwa. Katika kufafanua nadharia ya uhalisiya, Emmanuel Kant, Schiller, Flaubert, wanamtazama mtunzi kwa jicho la mbali zaidi. Mfano, mtoto anapokuwa mchezoni, hufanana na mtunzi ambaye huunda ulimwengu wake, au huvipanga upya vitu katika ulimwengu wake, ili vimpendeze. Kulingana na nadharia hii, mtunzi hufanya kazi yake sawa na mtoto

anayecheza, isipokuwa mtunzi hutumia visa. Kwa upande mwingine, mtunzi anafahamu kuwa hatarajiwi kuendelea kucheza au kuota, kama afanyavyo mtoto, bali hupaswa kutenda mambo kiuhalisiya na kiutu uzima. Baadhi ya matamanio yanahitaji kusitiriwa, yasijulikane kwa wengine, kwani huwa ni faragha nzito za kijamii. Kazi ya fasihi, kulingana na mtazamo huo, huwa ni jaribio la kutimiza matamanio ya mtunzi juu ya mambo anayoyaona ama kuyasikia ndani ya jamii yake na kutaka yasomwe katika uhalisiya huo huo wa kimafumbo.

Sengo (2009), Ntarangwi (2004), Emmanuel Kant (1790), Schiller (1798), Gustav Flaubert (1800) wanakubaliana kuwa, lengo la mtunzi wa kazi ya fasihi ni kuonesha ukweli jinsi ulivyo. Nadharia ya uhalisiya ilitusaidia wakati wa kujibu swali letu la pili, lililomtaka mtafiti kuchunguza ujumbe unaopatikana katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha. Mhalisia husadiki matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa katika uzoefu maishani. Nadharia ya uhalisiya ilitusaidia kupata ukweli kwamba, wanamke wa jamii ya Wanyiha, tangu jadi walipewa heshima na kuthaminiwa ni walezi wa familia na wachapa kazi. Uchumi wa Wanyiha umo mikononi mwa kina mama.

## 2.4 Hitimishi

Nadharia zilizofafanuliwa hapo juu zilitumika sambamba katika kukamilisha kazi ya utafiti huu. Nadharia hizo zilitumika katika vipengele tafauti tauti kulingana taalimu ya utafiti inavyoelekeza kuwa ukusanyaji wa data na uchambuzi wake ni lazima uongozwe na nadharia Kothari (2008). Nadharia ya ndani- nnje ilitumika katika hatua ya ukusanyaji wa data masikanini na nadharia ya Ufeminisit na Uhalisiya zilitumika katika hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Mbinu na njia za utafiti ni dhanna zinazofanya kazi kwa pamoja katika utafiti. Deusi (2011) anazitafautisha dhanna hizo kwa kusema kuwa, mbinu ni namna au jinsi ya mtu, anavyoweza kufanikisha jambo lake. Mbinu ya utafiti ni namna inayomwongoza mtafiti kuchunguza lake hadi akalipatia suluhu. Njia ni mpito wa kuimarishia mbinu. Bailey (1994) anasema, mbinu za utafiti ni hatua za kifalsafa za mtafiti, ambazo huzitumia katika kazi yake ya utafiti, na hasa namna atakavyokusanya data, kuzichambua na kuziandikia taarifa ya utafiti.

Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa, mbinu za utafiti, ni jumla ya taratibu zote zinazotakiwa kufuatwa katika kazi ya utafiti, njia ni mikakati anayotumia mtafiti ili kufanikisha lengo lake. Mbinu za utafiti zipo nyingi, ni pamoja na usaili, umakinifu, maswali na majibu, mahojiano na kusoma machapishi. Sevenye na Robinson (2001), wanasema, njia za utafiti, humsaidia mtafiti akubalike katika jamii na kupewa taarifa bila ya hofu. Katika utafiti huu, data iliyotumika ilitokana na taarifa na majibu ya maswali kadhaa yaliyoulizwa kwa watoa taarifa masikanini.

## 3.2 Njia Zilizotumika Katika Ukusanyaji wa Data

Kombo na Tromp (2006) wanasema, ukusanyaji wa data ni namna ya kutafuta taarifa mbalimbali zenye ukweli ndani yake kutoka kwa watafitiwa. Njia zilizotumika ni mahojiano, udurusu wa nyaraka maktabani, umakinifu na wasaidizi wa utafiti. Utafiti huu ni changamani, ulitumia njia hizo na kutuwezesha kukidhi matarajio ya utafiti.

### 3.2.1 Njia ya Mahojiano

Hii ni njia ya kupata data kwa kutumia maswali na majibu yanayotokana na mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa Kothari (2008). Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa katika njia hiyo, mtafiti lazima awe na mada maalumu itakayoongoza mahojiano hayo. Wanapendekeza, kuwa katika njia hiyo, kirimbo kitumike kwa ajili ya kurekodi mambo yote yatakayojadiliwa.

Kwa msingi huo, mtafiti aliweza kufanya mahojiano na kundi la watu lililoandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya maswali ya mahojiano hayo. Manufaa ya njia hii ni kwamba, humsaidia mtafiti kupata mawazo, mwelekeo na ufahamu wa wahojiwa. Baadhi ya maswali yaliyoulizwa ni; jee, vitendawili vya jamii ya Wanyiha vinamsawiri vipi mwanamke? Vitendawili hivyo vinawasilisha ujumbe gani kwa jamii?

### 3.2.2 Njia ya Umakinifu

Ni njia ambayo humwezesha mtafiti kuwamo ndani ya mazingira halisi ya upatikanaji wa data zinazohitajika. Leary (2001) anapendekeza kuwa, njia ya umakinifu ni nzuri zaidi kwani humfanya mtafiti kupata data katika mazingira halisi ya watafitiwa kwa kujionea mwenyewe ukweli wa jambo kama linavyoonekana katika udhati wake. Ingawa Kahn (2011) anasisitiza kwamba njia hii inafaa zaidi kutumika katika mambo ya kisayansi, lakini kwa Afrika, sayansi ilipewa kazi pana zaidi kuliko sayansi ya kiingereza, (ambayo kimsingi ni Kemia, Biolojia, na Fizikia). Njia hii ni mwafaka, tumeichagua kwa sababu, inayaweka wazi mazingira ya usimuliaji wa vitendawili.

### 3.2.3 Udurusu wa Nyaraka Maktabani

Udurusu wa nyaraka maktabani ni mbinu inayopendekezwa na Leary (2001) na Kumar (2010), wanasema kwamba zipo data ambazo huweza kupatika katika nyaraka zilizotunzwa maktabani na kwenye mitandao ya kielektroniki. Data hizo zinaweza kutumika katika kazi ya utafiti, jambo la msingi ni kwamba lazima pawepo na uhusiano wa mada. Katika utafiti huu baadhi ya data zilikusanywa kwa njia ya kusoma na kuchambua maandiko mbalimbali yanayohusiana na vitendawili. Ukusanyaji wa data hizo ulifanyika katika maktaba/makavazi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maktaba na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Sababu ya kuchagua maktaba hizi ni kwamba hizi ni miongoni mwa maktaba zenye nyaraka na taarifa au data nyingi zilizofanikisha utafiti huu kukamilika. Mbinu ya kudurusu maktabani humsaidia mtafiti kupata maelezo ya ziada yanayoshadidia data za msingi ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti huu.

## 3.3 Wasaidizi wa Ukusanyaji wa Data

Wasaidizi, katika kazi ya utafiti ni kundi la watu ambao ni wenyeji katika maeneo ya utafiti, ambao huongozana na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti. Mgogo (2012) anasema, tunalazimika kuomba wasaidizi ambao ni wenyeji wa eneo la kiutafiti ili kupunguza ugeni wa mtafiti. Kazi kubwa ya kundi hilo ni kumtambulisha mtafiti kwa watafitiwa, kuwashawishi watafitiwa wawe na ushirikiano na mtafiti, kupunguza hofu kwa watafitiwa kuhusu mtafiti na kuelekeza maeneo au watu wenye kuhifadhi data zinazotafutwa. Katika utafiti huu tulishirikiana na uongozi wa vijiji kupata wasaidizi wawili katika kila kijiji tulichokusanya data hizi. Tuli ambatana nao wakati wa kukusanya data. Kwa kuwa vitendawili ni sehemu njema ya utamaduni wa

jamii, tuliziomba Kamati za Utamaduni na Michezo vijijini, zikishirikiana na Wenyeviti wa Vitongoji ili kupata wasaidizi wenye sifa. Katika utafiti huu, tulipata wazawa wa maeneo husika, wenye uzoefu na kuwatambua watu wenye kuhifadhi data zinazotafutwa, kwani wao wanajuana kwa sifa, mielekeo na tabia.

## 3.4 Zana za Utafiti

Zana za utafiti ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti alivitumia katika kazi ya ukusanyaji wa data. Miongoni mwa vifaa hivyo, ni kalamu na karatasi, kamera, ngamizi, simu ya mkononi, na kirimbo.

### 3.4.1 Kalamu na Karatasi

Kalamu na karatasi ni nyenzo za kuandikiya na kuhifadhiya maandishi. Kothari (2004), anasema, kalamu na karatasi ni zana za msingi katika utafiti wowote wa kitaalimu. Vifaa hivyo vilitusaidia kunukuu na kuhifadhi baadhi ya kumbukumbu muhimu, kama vile, majina ya watafitiwa, tarehe ya kukutana, baadhi ya taarifa za mahojiano yetu na walengwa.

### 3.4.2 Kirimbo

Kirimbo ni kifaa kinachotumika kunasia sauti za watafitiwa masikanini. Tulikitumia kifaa hicho tulipokuwa tunakusanya data kwa njia ya mahojiano na uchunguzi makini. Taarifa zilizorekodiwa katika kirimbo, tulizitumia katika hatua ya uchambuzi wa data.

### 3.4.3 Simu ya Mkononi (Rukono)

Hiki ni kifaa cha mawasiliano kati ya mtafiti na watafitiwa. Tulikitumia kifaa hicho kufanya makubaliano ya muda na mahali pa kukutania ili kuweza kufanya

mahojiano. Katika mazingira hayo, simu ya mkononi, ilirahisisha zoezi la kukusanya data, kwani mambo mengi yalifanyika kwa misingi ya makubaliano maalumu, kati ya pande mbili, yaani mtafiti na watafitiwa.

### 3.4.4 Ngamizi

Ni kifaa kwa ajili ya kucharazia maandishi. Tulikitumia kifaa hicho katika mambo mawili; kwanza, kukusanyia data za upili katika wavupepe baada ya kuunganishwa katika mtandao, pili, tulikitumia wakati wa kuchapa ripoti ya tasnifu hii, ili iweze kusomeka katika maandishi.

## 3.5 Vyanzo vya Data

Data zilizotumika ndani ya kazi hii ni za aina mbili ; data zilizopatikana kutokana na mkusanyiko wa majibu ya moja kwa moja ya watafitiwa, ambazo huitwa data za msingi. Pili, data zilizopatikana kutokana na kutalii kazi tangulizi, ambazo huitwa data za upili, hupatikana katika vitabu, tasnifu, majarida, magazeti n.k.

### 3.5.1 Data za Msingi

Hizi ni data ambazo zilipatikana kutoka kwa watafitiwa baada ya kuulizwa maswali au kujadiliana na mtafiti juu ya mada ya utafiti huu. Kothari (2003) anasema, mtafiti huzikusanya mwenyewe kutoka masikanini. Masikanini ndiko wanakoishi watu. Kusiko watu k.v uwandani hakufanyiki utafiti wa kijamii. Katika utafiti huu, data zilizowasilishwa zilipatikana katika vijijiji vya Msia, Igamba, Wasa na Halambo.

### 3.5.2 Data za Upili

Hizi ni data ambazo zilipatikana katika machapisho, vikiwemo vitabu, majarida, tasnifu, nyavupepe, magazeti na matini zenye uhusiano na kazi hii. Kazi hiyo

ilifanywa na mtafiti ili kujiongezea maarifa na ujuzi wa kukamilisha utafiti huu. Mwali hufundwa na wajuzi watanguzi, watu wazima, wenye tajiriba za uhalisiya wa maisha.

## 3.6 Uteuzi wa Walengwa

Walengwa ni kundi dogo linalowakilisha kundi kubwa katika kazi ya utafiti. Creswell na mwenzake (2009), Kumar (2013), Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kwamba, walengwa ni kundi wakilishi la watafitiwa, linaloweza kutoa majibu ya maswali ya mtafiti. Webster (1985) anasema, kundi la walengwa ni kundi la watu wachache, lililoteuliwa kutoka katika kundi la watu wengi, kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Katika kazi za utafiti, walengwa hupatikana katika makundi tafautitafauti kama vile wanakijiji, wanafunzi, walimu, watumishi wa afya, madereva au mzawa yeyote n.k. Cohen na Lawrence (2000) na Bryman (2004) wanasisitiza kuwa, kiwango cha ukubwa wa walengwa, huamuliwa na mtafiti mwenyewe kutokana na sababu alizonazo. Miongoni mwa sababu hizo, ni aina ya utafiti, mada inayohusika, kiasi cha raslimali alizonazo mtafiti, raslimali zinazohusishwa ni muda, fedha wa vifaa vya kuendeshea utafiti. Katika utafiti huu, walengwa ni watu waliohifadhi vitendawili vya jamii ya Wanyiha.

### 3.6.1 Njia za Kupatia Walengwa

Katika kazi ya utafiti, zipo njia zinazopendekezwa na wataalamu ili zitumike kupata walengwa Tromp na Kombo (2006) wanapendekeza njia mbili. Njia ya kubahatisha ambayo mtu yeyote huingizwa katika kundi bila kutumia kigezo chochote. Njia ya matabaka, mtu huingizwa katika sampuli kulingana na vigezo vitakavyowekwa na mtafiti. Wanasisitiza kuwa, njia ya matabaka hutumika katika utafiti wa mambo ya

kale, au katika mada nyeti kama utoaji wa mimba, umalaya, magonjwa, watoto wa mitaani. Mada kama hizo zisipotafutiwa kundi maalumu la watafitiwa, ni rahisi sana, kwa mtafiti kushindwa kupata data halisi.

Katika utafiti huu, njia ya kimatabaka ilitumika, kwa sababu, siyo jambo rahisi kwa kila Mnyiha kuwa na uwezo wa kuhifadhi, kutega na kutegua vitendawili, bali raslimali hiyo ni kipawa cha watu wachache ambao, walipatikana, kwa ushirikiano kati ya mtafiti na wasaidizi wake kutoka katika kila kijiji kilichoteuriwa. Vijiji vinne vilifikiwa, katika Tarafa ya Igamba, kila Kijiji kilihusisha watafitiwa sita kwa kuzingatia jinsia. Hivyo, jumla ya watu ishirini na wanne walifikiwa, wanawake kumi na wawili na wanaume kumi na wawili. Kundi la watu hao, ndilo lilitega na kutegua vitendawili vilivyowasilishwa ndani ya tasnifu hii. Kielelezo hicho hapo chini kinaonesha mgawanyo wa watafitiwa kwa kuzingatia kigezo cha jinsia.

**Jedwali Na. 3.1: Uteuzi wa Wahojiwa**

| **Kijiji** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Halambo | 3 | 3 | 6 |
| Igamba | 3 | 3 | 6 |
| Msia | 3 | 3 | 6 |
| Wasa | 3 | 3 | 6 |
| **Jumla** | **12** | **12** | **24** |

Chanzo ni Mtafiti (2014)

### 3.6.2 Njia ya Uchambuzi wa Data

Kipengele cha uchambuzi wa data kinahitaji umakini, utulivu na ufahamu mkubwa. Katika hatua hii, mtafiti anashauriwa kuzingatia mambo muhimu matatu. Kombo na Tromp (2006), wanasema, kwanza ni lazima mtafiti azijue data zisizohitajika na

aziondoe katika uchambuzi wake. Kothari (2003) anasema, katika utafiti wa kiulimbe, baada ya kukusanya data, mtafiti anapaswa kuzichambua data hizo kulingana na matarajio ya utafiti huo. Uchambuzi humsaidia mtafiti kupata ukweli wa madhumuni aliyojiwekea. Beynon- Davies (2002), anasisitiza kuwa, data ipo ngazi ya chini, taarifa ni ngazi ya pili na hatimaye maarifa ni ngazi ya juu kati ya zote tatu. Ili data ibadilishwe kuwa taarifa, ni lazima ifasiliwe na kupatiwa maana, hatua hii huitwa uchambuzi wa data.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2003), wanasema data, hutoa jibu la swali la utafiti na ili matokeo ya utafiti yaweze kuaminika na kukubalika lazima yachambuliwe vizuri. Data za utafiti huwa nyingi na mara kadhaa huwa katika mchanganyiko mkubwa. Mtafiti hulazimika kuzichambua kwa umakini ili aweze kutoa taarifa kamili kwa wasomaji wa kazi hiyo, kulingana na lengo la kazi yake.

Best na Kahn, (1989) wanapendekeza njia zinazofaa kutumika katika uchambuzi wa data nazo ni; kutumia asilimia, endapo kuna idadi kubwa ya watafitiwa, kuchambua data kwa kutumia wastani, hutumika ili kuelewa watu wanasema nini juu ya jambo fulani, uchambuzi wa data kwa kigezo cha uwiano, hutumika ili kupata kiasi cha uhusiano wa ongezeko au upungufu wa kipengele kimoja dhidi ya kipengele kingine.

Hata hivyo, katika utafiti huu tumetumia njia ya kimaelezo ambayo inapendekezwa kutumika katika utafiti wa mambo ya sayansi ya kijamii Kothari (2008). Mkabala wa kimaelezo umetumika kwa sababu utafiti huu, hauhitaji data za uwiano na asilimia bali umejikita katika kutafuta maelezo ya kina, ukweli na uthibitishi. Mtafiti

aliongozwa na nadharia ya Ndani- nnje, Ufeministi na uhalisiya, kila moja ikitumika katika mazingira maalumu.

## 3.7 Hitimishi

Sura hii imeeleza kwa kina njia/mbinu zilizotumiwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Baadhi ya njia hizo, ni mahojiano pia kuna maelezo ya matumizi ya vifaa vilivyotusaidia katika upatikanaji na uhifadhi wa data zetu, miongoni mwa zana hizo ni, kirimbo, kalamu na karatasi. Baada ya kukamilisha sura tatu yenye mbinu za kukusanyia data, tunaingia sura ya nne yenye vipengele vya uwasilishaji na uchambuzi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amehudhurisha majibu ya maswali yaliyopatikana katika mahojiano pamoja na taarifa alizozipata katika majadiliano na uchunguzi makinifu, uliofanyika.

## 4.2 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji na uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika kazi yoyote ya utafiti, katika hatua hii mtafiti amewasilisha taarifa zilizokusanywa na kuzifanyia upembuzi makini kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu. Lengo kuu la utafiti ni kukusanya vitendawili, kuvianisha, kuvichunguza kwa undani na kuonesha namna vinavyowasawiri wahusika wanawake. Madhumuni maalumu ya utafiti yalikuwa ni; (a) Kutathimini usawiri wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha (b)Kuchunguza ujumbe unaopatikana katika vitendawili. Ili kufikia lengo la utafiti huu, maswali mawili yaliulizwa (a) Jee ni kwa namna gani, vitendawili vya Wanyiha huwasawiri wanawake? (b) Jee, ni ujumbe gani unaopatikana katika vitendawili vya Wanyiha?

Kabla ya kufikia hatua ya uwasilishaji wa data, hatua zifuatazo zilizingatiwa. Kwanza, mtafiti alirekodi vitendawili kwa kutumia kirimbo, vikiwa katika lugha ya Kinyiha, hatua ya pili ilikuwa ni kuvitarijimu kwa lugha ya Kiswahili, hatua ya tatu, ni kuonesha matukio muhimu katika vitendawili vilivyoteuliwa kuchunguzwa, hatua ya nne, ilikuwa ni kuchunguza namna mhusika mwanamke anavyosawiriwa na

ujumbe uliyofichwa na wahenga ndani ya vitendawili hivyo. Data zilizowasilishwa katika kazi hii ni matokeo ya taarifa za data zilizochambuliwa. Kila swali lililoulizwa katika hojaji za mtafiti limewasilishwa kwa kujitegemea. Swali la kwanza liliuliza, Jee ni kwa namna gani, vitendawili vya Wanyiha huwasawiri wanawake? Majibu ya swali hilo yalichambuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi inayojikita kufafanua mtazamo wa jamii ya Wanyiha kuhusu wanawake, nadharia ya uhalisiya msingi wake ni kupata uhalisiya wa hali halisi na nadharia ya ndani – nnje ni kuonesha undani wa jambo katika vipengele vya fani na maudhui.

## 4.3 Usawiri Chanya wa Mwanamke Katika Vitendawili vya Jamii ya Wanyiha

Vitendawili vilivyokusanywa na kupembuliwa kiutafiti katika jamii ya Wanyiha, tumetambua kuwa, fasihi ya Wanyiha kupitia kijitanzu cha vitendawili, humsawiri mwanamke katika mtazamo chanya, jambo hilo limejidhihirisha katika baadhi ya vitendawili vilivyokusanywa ndani ya jamii hiyo.

### 4.3.1 Mwanamke Anasawiriwa Kama Mama Mlezi wa Watoto Katika Jamii

Kitendawili katika lugha ya Wanyiha "*Umayi akujenda ni ng'ongo pansizyi". Jibu, inkozu.*

Tarjama ya kitendawili katika lugha ya Kiswahili

"Mama yangu anatembea na kibyongo. Jibu lake ni konokono

Kichocheo cha msingi, katika kitendawili hicho, ni "Mama kutembea na kibyongo" tarjama sahihi ya neno kibyongo Kamusi ya Oxford (1981), wanasema ni sehemu ya mgongo inayojitokeza nnje au nundu inayojitokeza sehemu ya mgongo katika mwili

wa binadamu, hayo ni maradhi au kilema kwa binadamu. Kibyongo kikimpata mwanadamu, huendelea kuishi nacho mpaka mwisho wa uhai wake. Jamii ya Wanyiha inanasibisha hali hiyo na malezi ya mama kwa mtoto wake, humlea tangu hatua ya uchanga hadi kifo chake, na hata baada mama kufariki duniya, uhusiano wa mzazi huyo na watoto huendeleya kwenye ndoto, duwa, mizimu na kumbukizi.

Kitendawili hicho kinamsawiri mwanamke akiwa ndiye mwenye nafasi kubwa ya malezi ya mtoto, mama huanza kulea mtoto na kutembea naye tangu siku ya kushika ujauzito. Katika kipindi hicho anahitaji kula vizuri, kupata muda wa kupumnzika, kupata tiba kwa muda sahihi, kuepuka kazi nzito na migogoro isiyokuwa ya lazima, mwanamke hutekeleza yote hayo akiwa na matumaini ya kujifungua mtoto kwa salama, mwenye afya njema, kimwili na kiakili. Mama akishajifungua, mtoto huendelea kuishi akimtegemea mama kwa chakula, kumstiri na baridi/ joto, kusimamia uhai na usalama, kumfundisha stadi ya kuzungumza, kumuelekeza na kumtambulisha vitu vinavyomzunguka. Katika jamii ya Wanyiha na nyingine nyingi za Kiafrika, mama anapaswa kuishi hivyo, huo ndiyo Uafrika wa kweli, upo tangu jadi ndiyo maana wahenga walinena, na bado inasemwa nani kama mama? Thamani ya mwanamama ni ya kipekee.

Mtoto haachani na mama yake, utafutaji wa riziki, wachumba na marafiki, mama huwa mstari wa mbele kupewa taarifa kabla ya baba. Unyihani, mtoto anapopata mchumba, mzazi wa kwanza kujulishwa ni mama, baada ya majadiliano ya hao wawili, baba ni wa pili kupewa taarifa hiyo, ambayo huipata kupitia kwa mama. Mtoto akiingia katika ndowa, hukumbana na misukosuko ya kiulimwengu, adha zikizidi, hukimbiliwa mama, ili kutafutwe ufumbuzi. Mtoto akitaka kufanya jambo

jema, lenye mafanikio, humshirikisha mama mzazi, japo kumpatia taarifa juu ya matarajio yake, ndiyo maana wanajadi waliibuka na usemi kwamba, "*Uchungu, wa mwana aujua mama",* wakati yote hayo yakifanyika, baba ni mshuhudiaji tu wa matokeo ya malezi ya mtoto. Hana uwezo wa kunyonyesha wala kushinda na mtoto kutwa nzima kama afanyavyo mama. Je mtoto awe mali ya mama au baba? Bila ya mbegu ya baba, ujauzito haupatikani. Mtoto akipatikana, akakuwa na akawa na fahamu zake, hatazamiwi kubaguwa wala kuchaguwa baba na mama, wote ndiwo wazazi wake, kila mmoja amebeba wajibu wake kijamii katika malezi na makuzi ya mtoto.

Jibu la kitendawili hicho konokono, limebeba falsafa kamili ya jamii ya Wanyiha kuhusu malezi ya mtoto. Mtoto akizaliwa anapaswa kubebwa na mama mgongoni, hiyo ni ishara ya upendo wa mama kwa mwanaye. Mtafitiwa wetu, Elizabeth Nzowa (2015 kijiji cha Igamba) anasema, mgongo wa mama ni Ikulu asiliya ya mtoto akikorofishwa, akibanwa na usingizi, akichapwa ama akifokewa, hutafuta mahali ulipo mgongo wa mama, akiamini kuwa, pale ni mahali salama kwake. Kitendawili kingine kinachomsawiri mwanamke kama mama mlezi katika lugha ya Kiswahili ni pamoja na – Mama hachoki kunibeba (Jibu-*kitanda*).

-Mama hatui mzigo wake ( Jibu- *konokono*)

### 4.3.2 Mwanamke Kiumbe Mvumilivu

Kitendawili katika lugha ya Wanyiha

"*Usokulu akuhomaga unyohokulu shima, ilelo atahepa narumo. (Jibu ni Ituli, numnsi)*

Tarjama ya kitendawili katika lugha ya kiswahili

“Babu humpiga bibi kila siku lakini hajawahi kuondoka (kukimbia)” Jibu, kinu na mchi wake (kitwangio).

Vichocheo vya msingi katika kitendawili hicho ni;

-Babu kumpiga bibi lakini hajawahi kukimbia au kutoroka

-Kinu na mchi (kitwangio).

Kitendawili hicho, humsawiri mwanamke, kama kiumbe mvumilivu katika shida anazozipata kutoka kwa mume wake. Kinu ni kifaa maalumu kinachotumika na wanawake, zaidi katika shughuli zao za kila siku, Kazi kubwa ya kinu ni kulainisha nafaka kama mihongo mikavu, mahindi makavu na viungo vya mboga ili viweze kupikwa kwa urahisi, pia kinaweza kutumika kwa ajili ya kutwangia dawa. Uhusiano wa kinu na mchi (kitwangio), mchi ni kipande maalumu cha mti kinachotumika kutwangia vitu kwenye kinu. Kinu ni chombo cha mti ambacho nafaka huwekwa ndani yake kisha, nafaka hutwangwa kwa kutumia mchi. Vifaa hivyo viwili, hufanya kazi kwa pamoja na hutegemeana. Katika falsafa ya mafumbo ya kiafrika, wakiwamo Wanyiha, mchi ni mume na kinu ni mke.

Jamii ya Wanyiha inalinganisha maisha ya wanandowa na uhusiano kati ya mchi na kinu, mchi ni nafasi ya baba na kinu ni nafasi ya mama katika familia. Mtwangaji wa nafaka hutumia nguvu zake zote, kunyanyua mchi na kuushusha ndani ya kinu, bila kujali misukosuko itakayotokea. Katika familia za Wanyiha, mama hukumbwa na magumu mengi, hupigwa, hutukanwa, hunyimwa haki za kumiliki mali, hufanyishwa kazi ngumu, huzaa na kulea. Hayo yeye huyafanya na mume wake asijali sana dhiki azipatazo mkuu mweziwe. Mke ni mwenza wake, ni binadamu anayestahiki kulindwa, kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake. Pamoja na magumu yote hayo,

mwanamke huendelea kuishi na mume wake na kumtimizia haki zote za msingi, huo ni moyo wa uvumilivu na ujasiri mkubwa ambao huoneshwa na mwanamke. Kama asemavyo Sengo, upumbavu wa mwanamke ndio dawa pekee ya kuzima moto wa ushenzi wa mwanaume (Sengo, 2015 darasani).

#### 4.3.3 Mwanamke Anastahiki Kupewa Hadhi Katika Jamii

Kitendawili katika lugha ya Wanyiha

*“Ubaba azenzile inyumba yilinamaziho gavhili, iziho lyoka akasite umayi, ilyamavho akasite ubaba ana indipapulu. Navuluga igodo, kila mntu akwanza avhe wakuwandilo kumtwalila, apo inkonzye vhuli ili numo atahagundule kuti namtalishe uvhunji kumntwalila?*

*(Jibu nkunyetula ivikombe vyonti vitatu, nkwinjila kwayi, nkumleshela shoka, nkusyala navyo vivhili, nkusogola navyo kwa baba, nkumleshela shoka, sheshasyala kwepw nashope kusogola kumwela nene).*

Tarjama ya kitendawili katika lugha ya Kiswahili

“Baba amejenga nyumba yenye vyumba viwili na sebule moja, chumba kimoja amelala mama, chumba cha pili amelala baba na sebuleni nimelala mimi. Nimeambiwa nitayarishe uji kwa ajili yangu mwenyewe na wazazi wangu (vikombe vitatu), lakini baba na mama kila mmoja anataka awe wa kwanza kupewa uji wake. Jee nitatumia njia gani katika kugawa uji huo ili kila mmoja aridhike kuwa alipewa upendeleo?

(Jibu, chukua vikombe vyote vitatu ingia katika chumba cha baba/ mama, unamwachia kimoja, unaondoka. Chukua viwili vilivyobaki, ingia navyo kwenye chumba cha pili, atakayepelekewa ataona umebeba vikombe viwili mkononi,

ataamini kuwa amepewa nafasi ya kwanza, kimoja kitakachobaki utakunywa mwenyewe).

Kichocheo cha msingi katika kitendawili hicho ni;

Kuwahudumia wazazi baba na mama, wakiwa katika vyumba tafautitafauti kwa sharti la nani awe wa kwanza kuhudumiwa, bila mwenzake kujua.

Katika kitendawili hicho kinamsawiri mwanamke, ni mzazi mwenye hadhi ya kipekee kwa watoto wake. Wanajadi wa Kinyiha, waliona kuwa, baba na mama wana nafasi sawa katika malezi na makuzi ya mtoto, vivyo hivyo, hata katika kuwahudumia wanastahili kuhudumiwa kwa misingi ya haki na usawa, bila ubaguzi. Kitendawili hicho kinamweka mwanamke katika mazingira ya kuthamaniwa sawa na mume wake. Jamii ya Wanyiha ilipiga hatua zaidi katika kutambua na kuthamini mchango wa mwanamke katika jamii. Baba na mama kwa pamoja, ndio taasisi yenye jina la familia.

Kitendawili katika lugha ya Kinyiha

*Nkwonka umayi, nkumwenya na kuminso = jibu amakwi gamakusu*

Tarjama ya kitendawili katika lugha ya Kiswahili

Nanyonya ziwa la mama na kumtazama usoni = Jibu miti ya matunda

Vichocheo vya msingi katika kitendawili hicho

- Kunyonya
- kumtazama mama usoni
- Mti wa matunda

Kitendawili hicho, ni msisitizo wa kile kilichotangulia. Jamii inakumbushwa kwamba, mama ana mchango wa ziada katika malezi, ni wajibu wa kila mwanadamu

kutoa shukrani za ziada kwa mama yake. Katika kitendawili hicho, kuna mambo matatu yanayobeba uzito kuhusu mwanamke. Wanadamu wote hutegemea maziwa ya mama kama chakula cha awali na muhimu katika makuzi ya mtoto, hutupatia kinga ya maradhi na ndicho chakula kikuu cha mtoto, utotoni. Jamii ya Wanyiha ina falsafa yake kuhusu mtoto anaponyonya maziwa ya mama. Uso wake, humwelekea mama kama ishara ya kutoa shukrani kwa ajili ya upendo. Baba hana uwezo huo. Lugha ya kisitiari inatumika, kunasibisha tukio la mtoto kunyonya na mtu anapochuma matunda mtini, macho huendelea kutazama juu ili kuona, kama kuna matunda mengine yaliyoiva ili aweze kuchuma, isitoshe wahenga walisema " kushukuru tafsiri yake ni kuomba zaidi"

Tangu jadi mgawanyo wa kazi katika jamii ya Wanyiha ulizingatia jinsia, wanaume walifanya kazi ya uwindaji na kutafuta chakula kwa ajili ya familia, wanawake walibaki nyumbani kwa ajili ya kupika na kulea watoto. Katika mazingira ya aina hiyo, wanawake walipata nafasi ya kuwa jirani zaidi kiuhusiano na watoto, baadhi ya huduma zilizotolewa na mama ni kama vile chakula, kuuguza, usafi wa mwili na mavazi, kuwapatia maadili, kuwapatia ulinzi na usalama. Wanaume hawakupata nafasi zaidi ya kushiriki kutoa huduma kama hizo. Jamii iliona haja, ya kutoa tunu ya usawiri chanya kwa mwanamke, kama ishara ya kuthamini mchango wake katika jamii.

### 4.3.4 Mwanamke ni Kiumbe Mchapakazi Katika Jamii

Kitendawili katika lugha ya Kinyiha.

*Ingawanyetula unyina, utangaleha umwana= Jibu ulyala ni nanyasyo*.

Tarjama katika lugha ya kiswahili.

Ukimchukua mama, beba na mtoto = Jibu sagio (mawe maalumu ya kusagia nafaka za ulezi, mtama au uwele)

Vichocheo vya msingi katika kitendawili hicho

-Mama na mtoto

-Mawe ya kusagia

Kitendawili hiki kinamsawiri mwanamke kama kiumbe mchapakazi katika jamii. Sagio ni jiwe maalumu linalotumiwa na Wanyiha wakati wa kusaga nafaka za ulezi, mtama na uwele. Mawe hayo yalitumika sana kabla ya ugunduzi wa mashine za kusagia nafaka. Katika mazingira mengine, bado mawe hayo yanatumika ili kuepuka gharama za mashineni. Katika jamii ya Wanyiha, kazi ya kusaga nafaka kwa kutumia njia hiyo, ilifanywa na wanawake tu na siyo wanaume. Kila familia ilikuwa na kifaa hicho, ambacho binti anapoolewa alipewa na wazazi wake kama kifaa maalumu cha kutayarishia unga wa nafaka. Mwanamke alipaswa kulinda na kukitumia kifaa hicho katika maisha yake yote. Kitendawili hicho ni kielezeo kinachoonesha baadhi ya shughuli muhimu za jadi zilizofanywa na wanawake wa Kinyiha. Kuna maelezo, ambayo bado, hayajathibitishwa kwamba, nafaka ikisagwa kwa kutumia njiya hiyo ya jadi, huhifadhi ladha halisi kuliko kusaga mashineni. Sababu moja ya haraka kuhusu unga wa mashineni ni kwamba, unaweza kuwa na harufu ya mafuta au vipande vya chuma ambavyo ni hatari katika afya ya binadamu.

Mchango wa wanawake katika uwajibikaji kazini katika jamii ya Wanyiha, ni jambo ambalo limepewa uzito na watafiti waliotutangulia Unyihani. Mgogo (2012) anasema, wanawake wapo mstari wa mbele kuhifadhi na kudumisha tanzu za fasihi simulizi, wakati wa ukusanyaji wa data, idadi kubwa ya data zilizotumika katika

utafiti wake, zilikusanywa kutoka katika kundi la wanawake, mchango wa wanaume ulikuwa ni mdogo sana. Maelezo hayo ni ushahidi kwamba, wanawake katika jamii ya Wanyiha, wapo mstari wa mbele kujituma katika utekelezaji wa mambo yote yanayowahusu wao kama sehemu ya jamii. Katika utafiti huu jambo hilo limejidhirisha, washiriki na wategaji na watenguaji wengi wa vitendawili, walikuwa ni wanawake.

Suala la mwanamke wa Kitanzania, kusawiriwa kama mchapakazi, limejitokeza hata katika kazi za fasihi andishi, Mbogo (2005), anamsawiri Mama Ntilie kama mwakilishi wa wanawake wanaofanya kazi kwa bidii ili kujipatia kipato kwa ajili ya malezi ya familia. Katika mazingira ya kawaida, sehemu nyingi za biashara ndogo ndogo, humilikiwa na kuendeshwa na wanawake zaidi kuliko wanaume, sehemu za vijijini, wanawake hufanya kazi za shambani pamoja na wanaume, pia hufanya kazi za ziada, kama kuokota kuni, kuteka maji, kufua na kutunza nyumba, kukata nyasi za kuezekea nyumba. Hizo ni shughuli ambazo ni nadra sana kuona wanaume wakizifanya.Kila yalipobidi yalifanyika.

Kwa upande mwingine, kitendawili hicho kinamsawiri mwanamke kama mama mlezi wa watoto, dhanna ambayo, imeijadiliwa kwa upana katika kipengele cha 4.4.1. Jambo la msingi hapo ni kwamba, mama kamwe hawezi kujitenga na mtoto wake katika malezi, hata kama hilo likitokea, mtoto huyo, atalelewa na mama mwingine kama kitendawili kinavyosisitiza kuwa, ukibeba jiwe lazima uchukue na sagio lake. Katika utafiti huu, ambao uchambuzi wake umeongozwa na nadharia ya ufeministi na uhalisiya, kwa kiasi kikubwa data zimeonesha kuwa, katika jamii ya Wanyiha, malezi ya watoto, yalisimamiwa zaidi na wanawake, kuliko wanaume.

Hata hivyo, suala ya usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi simulizi, linapaswa kutazamwa kwa umakini mkubwa na kuzingatia matakwa ya wanajamii kama anavyotukumbusha Sengo (2009) kuwa, fasihi ina kwao. Mfano Nicholaus (2011), alifanya utafiti wa usawiri wa jinsia katika vitendawili vya jamii ya Vwasu wanaoishi katika wilaya ya Mwanga na Same mkoa wa Kilimanjaro, alitumia kitendawili cha "*Kaka aninka ivindi narera laoka nzao" (iasha la mghuva)* alitoa tarjama katika lugha ya Kiswahili kuwa, "Ukichukua mwana chukua na mtoto = jibu ni sagio" Anasema kuwa, usawiri katika kitendawili hicho, ni mwanamke kama mama mzazi na mlezi.

Hata hivyo, maelezo yake yanatuchanganya, anapoendelea kusema kuwa, kwa upande mwingine, kitendawili hicho humsawiri mwanamke kama kiumbe duni. Uduni anaousema, ni akili ya mama kufananishwa na akili ya mtoto, eti kwa kuwa, wanaambatana pamoja muda wote. Huo siyo uduni ni maumbile ya kiushunuzi, mama humudu kulea vichanga na watoto wadogo sana, ni uwezo ambao baba kanyimwa.

Jamii ya Wanyiha hukitumia kitendawili hicho hicho lakini wao, humsawiri "mwanamke kama kiumbe chenye uwezo wa kufanya kazi". Siyo lengo ya mtafiti kutafuta makosa ya wanazuoni waliotutangulia, lahasha! Lengo ni kushadidiya hoja za wanazuoni, Sengo (2014 darasani) anasema kuwa, kazi za fasihi simulizi hutawaliwa na ncha saba ambazo zinaweza kuathiri maudhui ya kazi hizo.

Tafauti ya wahusika

Tafauti ya hadhira

Tafauti ya fanani

Tafauti ya wakati

Tafauti ya wanajamii

Tafauti ya shughuli za wanajamii

Tafauti ya malengo ya usimuliaji.

Kipengele hiki kilikuwa kinatoa majibu ya swali letu la kwanza katika utafiti wetu lililouliza, Jee, ni kwa namna gani, vitendawili vya jamii ya Wanyiha huwasawiri wanawake? Maelezo yaliyowasiliswa katika sehemu hiyo, ni majibu yaliyopatikana kutoka kwa watafitiwa. Katika kijitanzu cha vitendawili, imeonekana kuwa, mwanamke ni mzazi na mlezi wa jamii, mwanamke ni mvumilivu, mwanamke ana hadhi tafauti na ya mwanaume na mwanamke ni mchapakazi. Usawiri chanya uliowasilishwa katika utafiti huu haujaitalii jamii nzima na vijitanzu vyote vya fasihi katika jamii ya Wanyiha. Mzamo wa kiuwanazuoni unahitajika zaidi, ili kuendelea kupembua, taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi. Kwenye jadi ya Wanyiha. Sifa kubwa ya kipekee ya wanamama wa kinyiha, ni kukubali kuolewa wengi kwa mume mmoja wakizingatia wingi wao katika jamii, na ni haki ya kila mmoja wao.

### 4.3.5 Ujumbe Unaopatikana Katika Vitendawili vya Wanyiha

Katika sehemu hii, tumehudhurisha majibu ya swali letu la pili lililouliza, Jee, ni ujumbe gani unaopatikana katika vitendawili vya Wanyiha? Wahakiki wa kazi za fasihi kama vile, Nkwera (1978), Sengo (1985), Mlacha na Madumulla (1991), Msokile (1993), Mulokozi (1996), Senkoro (2006), Wamitila (2008), wanakubaliana kwamba, ujumbe ni miongoni mwa vipengele vinavyotokana kipengele cha maudhui katika kazi za fasihi. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988) wanasema kuwa, ujumbe ni fundisho amabalo kazi ya fasihi huwasilisha kwa hadhira yake. Ujumbe katika kazi

za fasihi huwa na lengo tafauti tafauti, unaweza kuonya, kuadilisha, kutoa taarifa kuhusu mgongano fulani n.k. Tunaweza kusema kuwa, katika kazi za fasihi, ujumbe ndicho kipengele kinachobeba uzito wa maudhui yote yanayozungumzwa ndani ya hadithi, semi, ushairi, riwaya kwani lengo kuu la kazi za fasihi, ni kuelimisha jamii juu ya kuwa na furaha ya pamoja ya maisha ya kila siku. Katika utafiti huu, tumepembua kwa kina, ujumbe unaopatikana katika vitendawili vine vya jamii ya Wanyiha. Vitendawili hivyo, ni vile vinavyomsawiri mwanamke katika mtazamo chanya, uchambuzi wake uliongozwa na nadharia ya Uhalisiya.

#### 4.3.5.1 Mama ni Mlezi wa Watoto

Kitendawili katika lugha ya Wanyiha

"*Umayi akujenda ni ng'ongo pansizi". Jibu, inkozu*

Tarjama ya kitendawili katika lugha ya Kiswahili

"Mama anatembea na kibyongo" Jibu lake ni konokono

Kichocheo cha msingi katika kitendawili hicho ni

"Mama kutembea na kibyongo"

Ujumbe unaojitokeza ni malezi ya mama kwa watoto. Kitendawili hicho kimeongozwa na lugha ya sitiari, mama anatembea na kibyongo, jibu lake ni konokono. Matumizi ya sitiari ni miongoni mwa sifa muhimu za vitendawili Senkoro (1985). Ujumbe unaojitokeza katika kitendawili hicho ni kwamba, mwanamke anatambulishwa wajibu alionao wa malezi ya mtoto. Mama anawajibika kumbeba mtoto wake mgongoni na kutembea naye popote anapokwenda, kama konokono anavyotembea na mzigo wake mgongoni. Jambo hilo linasisitizwa kwa sababu, mtoto anahitaji uangalizi, upendo na malezi ya mara kwa mara kutoka kwa wazazi

ambao ndiwo waliomleta hapa duniani. Katika jamii ya Wanyiha na nyingine za Kiafrika, mama hubeba wajibu huo, hutembea na mtoto mgongoni na kuhakikisha kwamba, anamtimizia mahitaji yote muhimu, ya chakula, usafi wa mwili na mavazi na kulinda usalama wa mtoto.

“Mlemavu wa kibyongo huvumilia mateso ya kilema chake”, Ujumbe ni wa mama, anapewa hadhari awe mvumilivu katika malezi ya mtoto wake. Sifa kubwa ya mtoto ni kukosa utambuzi kuhusu mema na mabaya, mama hufanya kazi kubwa ya kumfundisha mtoto kutambua malimwengu kadha wa kadha yanayomzunguka katika maisha ya kila siku. Mtoto anaweza kuyakubali moja kwa moja au akayakataa kuyafuata mara moja, mama hapaswi kuchoka wala kukata tamaa kumfundisha mwanaye, hilo likipuuzwa, mabaya humpata mtoto, jamii huhitimisha na methali isemayo, “*asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu*” hapo mtafiti anajiuliza, mtoto ndiye mwenye kuonekana na kosa, jee ni kwanini mama abebe lawama? Hata hivyo, ingawa kitendawili na methali vinawalenga akina mama peke yao, kiundani malezi ya watoto, ni ya jamii kwa jumla, kila mwanajamii, kwa nafasi yake, ashiriki kikamilifu katika malezi ya watoto, kwani watoto huandaliwa kwa ajili ya kuitumikia jamii nzima.

Ujumbe mwingine wa kitendawili hicho ni kwmba, kulingana na falsafa ya Wanyiha katika malezi ya watoto, mtoto hubebwa na mama yake mgongoni kwa kutumia kipande cha nguo. Katika ulimwengu wa leo, ambapo kumekuwa na mwingiliano wa tamaduni za jamii tafauti tafauti, akina mama wasiige kila jambo wanaloliona, kila jambo huchipuka, hustawi na kutumika kulingana na matakwa ya wanajamii

wenyewe. Kwa sasa tunashuhudia akina mama, akina dada barabarani na mitaani, wameshona mifuko ya kuwatumbukiza watoto na kuwaweka vifuani kama nyani anavyobeba mtoto wake mwituni, wengine wamewatengenezea vitoroli, huwatumbukiza watoto wao na kuwasukuma kama mizigo au takataka zinazopelekwa jalalani, jee, hiyo ni falsafa ya wapi katika malezi ya watoto? vitendawili ni maktaba inayohusu jadi ya watu, jee, ni kitendawili kipi cha Kiafrika kinachoshadidiya hoja ya kubeba watoto kwenye mifuko, vifuani au kuwasukuma kwenye matoroli? Nyigenyige ni saratani ya ubongo inayouwa uwezo wa fikira na kuondosha thamani ya utu na ubinadamu.

#### 4.3.5.2 Mwanamke ni Mvumilivu Katika Jamii

"*Usokulu akuhomaga unyohokulu shima, ilelo atahepa narumo. (Jibu ni Ituli numnsi)*

Tarjama ya kitendawili kwa lugha ya kiswahili

"Babu humpiga bibi kila siku, lakini hajawahi kuondoka (kukimbia)"

Jibu, kinu na mchi wake (kitwangio)

Vichocheo vya msingi katika kitendawili hicho ni;

-Babu kumpiga bibi lakini hajawahi kuondoka

-kinu na mchi.

Ujumbe unaopatikana katika kitendawili hicho ni suala la uvumilivu wa mwanamke katika familia. Katika jamii ya Wanyiha uvumilivu wa mwanamke unaweza kutazamwa katika vipengele viwili vikubwa; uvumilivu kwa mume wake na katika malezi ya watoto.

#### 4.3.5.3 Mwanamke ni Mvumilivu kwa Mume Wake

Katika jamii ya Wanyiha na nyingi nyingine za Tanzania, imezoeleka kwamba, mwanaume ndiye mlezi mkuu wa familia na mambo yote huongozwa na naye. Jambo hilo linafasiriwa na wanaharakati wa haki za wanawake kuwa, ni mfumo dume. Katika mfumo huo, mwanaume ndiye mwenye madaraka ya juu, ya mambo yote ya kijamii, kiuchumi. Mfano suala la kuoa mitala ni jambo la kawaida kwa Wanyiha. Mke haulizwi na mume wake iwapo anahitaji mwanamke mwenzake kuchangia mume au la, mwanaume ataoa mwanamke bila kipingamizi chochote cha kijamii. Katika mazingira hayo, mke wa kwanza hawezi kukimbia ndowa yake, huendelea na maisha yake ya kawaida. Katika jamii ya Wanyiha mwanamke haruhusiwi kumrudishia mume wake kofi au ngumi hata kama ana uwezo huo. Ni utovu wa adabu na heshima. Ni hekima na busara ya kulea ndowa na familiya kwani mama ni mlezi wa familiya yote, watoto na mume wake.

#### 4.3.5.4 Uvumilivu Kipindi Cha Malezi ya Mtoto

Kutokana na mgawanyo wa kazi za kijamii, katika familia, mwanamke ana nafasi kubwa ya kushiriki katika malezi ya mtoto kuliko mwanaume. Muda wake mwingi huongozana na watoto wake katika sehemu anazofanya kazi zake. Ni wazi kuwa, adhaa nyingi zinazomkuta mtoto, hushuhudiwa na kutatuliwa na mama zao. Mama huonesha hali ya uvumilivu kwa mtoto wake tangu siku ya utungo wa mimba hadi siku ya kujifungua. Hicho ni kipindi kigumu kwa mwanamke. Ndani ya bibilia tunajifunza, kwamba adhabu kubwa aliyopewa mwanadamu baada ya kumuasi Mungu ni kuzaa kwa uchungu na Adamu utakula kwa jasho (Mwanzo 3:16-19), Wanasaikolojia wanasema kipindi cha ujauzito, mwanamke hufanya mambo yake

mengi bila kutumia akili yake ya kawaida aliyoizoea. Huwa na mihemuko ya kipekee kulingana na uhalisiha wa ujauzito.

Baada ya kujifungua, maisha ya mtoto hutegemea akili na uangalizi wa mama zaidi kuliko wa binadamu mwingine yeyote, ni kipindi ambacho mama husongwa na kazi nyingi zaidi, huduma za mama kwa mtoto zinahitaji uvumilivu mkubwa, kuandaa chakula kila kinapohitajika, kufanya usafi wa nguo kila zinapokuwa chafu, kumbembeleza kila anapohitaji kubembelezwa, kukesha usiku kucha kila anapougua, kuwapo kwa kazi hizo za mtoto, siyo kigezo cha kupumnzika kushiriki katika shughuli nyingine za kila siku katika familia. Kupika, kulima, kuvuna, kuokota kuni, kufua nguo za mume wake, za watoto wake, kuhudhuria katika matukio ya kijamii kama kuona wagonjwa, kushiriki katika misiba. Mambo yote hayo hufanywa na mwanamke katika hali ya uvumilivu mkubwa.

Mtafiti, alimuuliza mtafitiwa Maines Mwamengo wa kijiji cha Wasa 2014, iwapo uvumilivu huo hufanywa na mwanake kwa hiyari yake mwenyewe au ni shinikizo la kijamii. Mtafitiwa alieleza kwamba, uvumilivu wa mwanamke kwa mume wake ni jambo la kimazoweya, ambalo lipo ndani ya mfumo wa maisha ya Wanyiha, wanawake tunatambua kwamba tunaonewa, hatuna la kufanya, kwa sababu, tukipeleka malalamiko kwa mama zetu, kuhusu mateso tunayopata kwa waume zetu, tunaambiwa vumilieni, hata mimi naishi hivyo hivyo na baba yako. Lakini katika mazingira ya leo, wanawake hawana uvumilivu kama sisi watu wa zamani, baadhi ya wanawake hupigana au huwapiga waume zao. Baadhi ya wanaume wanashiriki vyema katika malezi ya watoto kwa kuwapunguzia baadhi ya kazi wake zao, k.v mashineni wanaenda na baiskeli au pikipiki, kuvuna mazao shambani wanashirikiana

kwa pamoja na kusomba kwa kutumia vyombo vya moto vya kukodi au vile wanavyomiliki, huchimba visima majumbani mwao, husomba kuni kwa kutumia wanyama kazi n.k.

Hata hivyo wanaume wasitumie kigezo cha uvumilivu wa mwanamke kama njia ya kuwanyanyasa na kuwanyima haki zao za msingi. Jamii huongozwa na mfumo wa maisha ya watu, Tanzania ya leo inaongozwa na misingi ya haki na usawa, baadhi ya taratibu zilizozoeleka kwa miaka mingi, tunapaswa kuzirekebisha kulingana na uhalisiya wa maisha ya watu waliopo kwa sasa. Tukiendelea kung'ang'ania kuishi kimazoea, mivutano ya kijamii haiwezi kuisha kamwe. Waneni hunena *hakuna marefu yasiyokuwa na ncha. Marefu huisha kwa watu kufuwata hekima za kwao, si za kuiga.*

**4.3.5.5 Mwanamke ni Mzazi Anayestahiki Kupewa Hadhi**

Kitendawili katika lugha ya Wanyiha

*"Ubaba azenzile inyumba yilinamaziho gavhili, iziho lyoka akasite umayi, ilyamavho akasite ubaba ana indipapulu. Navuluga igodo, kila mntu akwanza avhe wakuwandilo kumtwalila, apo inkonzye vhuli ili numo atahagundule kuti namtalishe uvhunji kumntwalila? (Jibu nkunyetula ivikombe vyonti vitatu, nkwinjila kwayi, nkumleshela shoka, nkusyala navyo vivhili, nkusogola navyo kwa baba, nkumleshela shoka, sheshasyala kwepw nashope kusogola kumwela nene).*

Kichocheo cha msingi katika kitendawili hicho ni;

Kuwahudumia wazazi baba na mama, wakiwa katika vyumba tafauti tafauti kwa sharti la nani awe wa kwanza kuhumiwa, bila mwenzake kujua.

Kitendawili hicho kinatoa ujumbe kwamba, mwanamke anasitahahiki kupewa hadhi katika familia/jamii. Mtazamo huo ni tafauti na kazi zilizofanywa na watafiti wengine wa Kiafrika, Ade (1983), Brigid (1994), Kipkorir (2004), Senkoro (2011), Lyatuu (2011), na Mbiu (2013). Wao wanaona kuwa wanawake hupewa mtazamo hasi ukilinganisha na wanaume, hivyo hawastahiki kupewa hadhi sawa kijamii. Katika maisha ya kawaida, mtoto anapaswa kulelewa na na wazazi, yaani baba na mama kwa pamoja, hivyo mtoto anawajibu wa kutoa zawadi kwa wazazi wake wote kama ishara ya kuwashukuru kutokana na malezi yao, jambo hilo anapaswa kulifanya kwa wazazi wote wawili bila ubaguzi wa aina yoyote kwa sababu, katika nyakati tafauti tafauti kila mzazi alitoa mchango wa malezi ambayo yamemsaidia mtoto katika kipindi cha makuzi yake.

Katika jamii ya Wanyiha, watoto huwaheshimu sana mama zao, jamii huamini kuwa, laana ya kutoka kwa mama huwa na nguvu zaidi kuliko inayotoka kwa baba. Taarifa za matatizo au mafanikio ya maisha ya watoto, hupelekewa mama kwa siri kabla baba hajajulishwa. Hiyo ni ishara ya wazi kwamba, watoto hujenga mahusiano ya karibu zaidi na mama zao, kwa kuwaona wanauwezo mkubwa wa kutatua shida zao.

Suala la mtazamo chanya wa mwanamke siyo jambo geni sana katika jamii zetu, Engles (1972) anasema, tangu jadi, kipindi cha utangu jamii ziliishi bila matabaka, mwanamke alikuwa na nguvu sawa na mwanaume, hata katika suala la madaraka, walishirikishwa. Matabaka ya kijamii ni matokeo ya maendeleo na mwingiliano kati ya jamii moja na nyingine. Jambo hilo linapewa nguvu na Red (1970), Bay (1976), Liwewa (1998), wote wanakubaliana kuwa, suala la ubaguzi kati ya mwanaume na mwanamke ni matokeo ya maendeleo ya jamii, mwanamke aliwekwa katika daraja la

kumtumikia mwanamume. Kuja kwa wa wakoloni kuliimarisha ubaguzi wa mwanamke kwa kutumia kigezo cha dini na elimu. Dini ya Kikristu inamtuhumu mwanamke kuwa ni chanzo cha maovu ya duniani na elimu aliyopewa ilikuwa ni duni ikilinganishwa na ya mwanaume. Kutokana na ushahidi huo, ni wazi kwamba, kitendawili hicho kiliibuka tangu kipindi cha maisha ya utangu.

#### 4.3.5.6 Mwanamke ni Mchapakazi Katika Jamii

Kitendawili katika lugha ya Kinyiha.

*Ingawanyetula unyina, utangaleha umwana= Jibu ulwala ni nanyasyo* .

Tarjama katika lugha ya kiswahili.

Ukimchukua mama, beba na mtoto = Jibu sagio (mawe maalumu ya kusagia nafaka za ulezi, mtama au uwele)

Vichocheo vya msingi katika kitendawili hicho

- Mama na mtoto

-Mawe ya kusagia

Ujumbe unaopatikana katika kitendawili hicho, ni nafasi ya mwanamke katika utendaji kazi kijamii. Heshima ya wanadamu wote ulimwenguni, hutokana na shughuli anayoifanya, kipimo cha utu wa mwanadamu ni kazi. Katika jamii ya Wanyiha, wanawake walitengewa baadhi ya kazi ambazo zilitumika kama kipimo cha kutambua ukamilifu wao kabla ya kuingia katika maisha ya ndowa. Baadhi ya kazi hizo ni; kuokota kuni, kuteka maji, kupika, usafi wa nyumba, kubembeleza watoto pamoja na kusaga nafaka katika sagio maalumu zilizotengenezwa kwa kutumia mawe. Kusaga nafaka za ulezi, za mtama na za uwele ilikuwa ni ishara ya

kujimudu katika kuandaa chakula cha familia. Shughuli zilizoorodheshwa hapo juu, zilikuwa ni kazi za ziada, kwa mwanamke.

Katika mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa, utafiti ulibaini kuwa, hata suala la mitala katika jamii ya Wanyiha, msingi wake ni utendaji bora wa kazi unaooneshwa na wanawake. Katika jamii ya Wanyiha, wanaume huwategemea wanawake katika shughuli za kilimo na sifa kubwa ya wanawake hao ni uvumilivu na bidii ya kazi. Raiton Silwimba (2014), anasema kwamba, mwanaume mwenye wake wengi, alihesabika kama tajiri, kwa sababu, wanawake walitumika kama vitendea kazi. Mwanaume mwenye wake wengi, mara nyingi, hakushiriki moja kwa moja katika kazi za kilimo. Mchango wake katika kilimo ulikuwa ni kutafuta maeneo mazuri yenye rutuba na kuwaonesha wake zake na watoto kama watendaji wakuu katika kilimo. Hata hivyo katika maisha ya sasa, hali hiyo imekuwa ikibadiIika taratibu, ndowa za mitala zinapungua, pengine ni kutokana na kuwapo kwa magonjwa ya kuambukizana maradhi ya UKIMWI, kuingia kwa imani ya dini za Kikiristu zinazosisitiza mke mmoja, mume mmoja, kwa hiyo, suala la kazi za kilimo, limekuwa ni la kusaidiana kati ya mwanaume na mwanamke, huo ni mwelekeo wa kumkomboa mwanamke wa Kinyiha kutoka katika hali ya kusimamishwa kipekee, katika kazi za kilimo.

## 4.4 Hitimishi

Katika kipengele hiki, tumeonesha baadhi ya ujumbe unaojitokeza katika vitendawili vinavyowasawiri wanawake kwa mtazamo chanya pekee. Ujumbe uliyopatikana ni maelekezo ya kuwa, wanawake ni watendaji kazi wakubwa zaidi kuliko wanaume. Wanaume tusiwadharau wanawake. Wao wana nafasi kubwa zaidi kijamii.

Mwanamke ni mvumilivu na mlezi wa watoto, watoto hao ni pamoja wanaume wote. Ni wajibu wa kila mtu katika jamii kutambua na kuthamini mchango chanya unaofanywa na mwanamke katika jamii zetu. Vyeo tisa vya Profesa Sengo alivyoviainisha vya mwanamke wa Kiafrika, kwamba yeye ni mama, nani kama mama? Yeye ni dada, fupi asiyetiiwa na kuthaminiwa na kaka zake wote? Yeye ni binti wa baba, kwamba ni mdogo wa mama wa baba? Yeye ni mke, waziri mkuu wa ndowa zote? Yeye ni shangazi, baba wa kike, huku yuko kule yuko. Kuna mtoto wababa, wa kakaake atakayethubutu kumnyanyasa? Yeye ni nyanya, malkiya dikiteta wa uzawa. Yeye mkwe, mke wa mjomba. Yeye ni mamamkwe (ama kaozesha binti yake, ama kaolewa yeye na mtoto wa baba au mama, ni shemeji, wote wawili) na mwisho yeye ni shemeji, (mke wa kaka au wa mama—ndugu mdogo wa kaka). Kwa vyeo vyote hivi ailani, mwanamke kapewa haki kubwa mno. Baada ya kukamilisha uchambuzi wa data sura hii, sura inayofuata tumezungumzia kuhusu maoni na mapendekezo katika tafiti zijazo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii kuna muhtasari wa kazi nzima, matokeo ya utafiti yameelezwa kwa kifupi pamoja na mapendekezo yaliyopatikana kwa watafitiwa, kuna mapendekezo serikalini, mapendekezo kwa ajili ya jamii nzima.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti Huu

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamke katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha. Utafiti uliongozwa na madhumuni maalumu madhumuni ya kwanza, yalikuwa ni kubainisha namna usawiri wa mwanamke unavyojitokeza katika vitendawili vya jamii ya Wanyiha na madhumuni ya pili lilikuwa ni kueleza ujumbe unaopatikana katika vitendawli vya jamii ya Wanyiha. Ili kufikia madhumuni hayo utafiti, vitendawili arubaini na majibu yake, vilikusanywa kutoka katika vijiji vya Halambo, Msia, Igamba na Wasa. Vitendawili vitano viliteuliwa kwa ajili ya kufanikisha madhumuni maalumu ya utafiti huu.

### 5.2.1 Usawiri Chanya wa Mwanamke

Utafiti huu umebaini kuwa, katika jamii ya Wanyiha, vipo vitendawili ambavyo humsawiri mwanamke katika mtazamo chanya, mwanamke anapewa uwezo wa kutenda mambo kama mwanaume. Jamii ya Wanyiha, inakubali kwamba, mwanamke ni mvumilivu katika adha za maisha, mwanamke ni mlezi mwenye uwezo wa kumtimizia mtoto mahitaji yake muhimu, mwanamke anastahiki kuthaminiwa kipekee. Kutokana na majibu ya utafiti huu, ni wazi kuwa, iwapo jamii

ya Wanyiha ingezingatia maadili yaliyomo katika vitendawili hivyo, mivutano isiyokuwa ya lazima kati ya mwanamke na mwanaume ingepungua kwa sababu kila jinsi ingejuwa nafasi yake na wajibu wake kijamii.

### 5.2.2 Ujumbe Katika Vitendawili vya Jamii ya Wanyiha

Vitendawili vilivyopata nafasi ya kupembuliwa katika utafiti huu, vimeonesha kuwa, ndani yake mna maelekezo, maonyo, tahadhari kuhusu maisha ya watu na shughuli zao. Ujumbe uliopatikana katika vitendawili vilivyoteuliwa, umejikita katika misingi ya kuiasa jamii. Katika mazingira halisi, mwanamke ni shupavu na akipewa nafasi ya kutenda jambo fulani anaweza, ndiyo maana, jamii ya Wanyiha imebainisha kuwa, mwanamke anaweza kufanya kazi za mikono, malezi ya watoto, ni uvumilivu na kupewa nafasi sawa ya kuthaminiwa kijamii kutokana na mchango wa mambo anayoyafanya.

## 5.3 Mambo Mapya Katika Utafiti Huu

Matokeo katika utafiti huu yameonesha kuwa, mwanamke ni kiumbe kilichokamilika na chenye uwezo wa kufanya kazi kipekee kwa kujiamini, kujituma na kujitambua. Matokeo hayo ni tafauti na kazi nyingine za fasihi simulizi zilizofanywa na Senkoro (1982 na 2011), Matteru (1982), Mbughuni (1982), Brigid (1994), Liwewa (1998), Lugano (1999), Ndungo (2006), Lyatuu, Alemu (2006),  (2011), Murikarika (2011) na Kitundu (2012) wao waliona kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe chenye hadhi duni ukilinganisha na mwanaume. Kuwepo kwa taouti za matokeo ya tafiti hizo kutokana na tofauti za kijamii, kijiografia, kihistoria, kiutamaduni, kiimani, kifalsafa na kimazingira.

## 5.4 Mapendekezo

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Wanazuoni

Utafiti huu ulijikita kuchunguza usawiri chanya wa wahusika wanawake katika jamii ya Wanyiha, bado kuna wahusika wengine kama wanaume, wanyama, mimea ambao wanaweza kuchunguzwa namna wanavyotumika katika ujenzi wa dhamira katika vitendawili. Kipengele cha maudhui tumeshughulikia ujumbe peke yake, bado kuna vipengele vingine ambavyo vinahitaji kuchunguzwa k.v Falsafa na dhamira.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa wanajamii

Jamii zetu ndogo ndogo za Wanyiha, Wazaramo, Wasukuma, Wagogo, Waha n.k zipange mikakati ya kulinda na kuendeleza utamaduni wao wenyewe, badala ya kuitegemea serikali kuu. Waanzishe vituo vya kuhifadhi mambo ya jadi kama vile, vitendawili, nyimbo, ngoma, uhamasishaji uanzie katika ngazi za vitongoji na vijiji, kwa kuafanya hivyo, wataendelea kurithishana kutoka kizazi kimoja hadi kingine na misingi ya jadi zao haitapotea.

### 5.4.3 Mapendekezo Serikalini

Serikali iangalie namna ya kuendeleza vituo vya kitamaduni katika ngazi za Mikoa ili viweze kutumika kama hifadhi ya utamaduni wetu wa asili kama ilivyo Bujora Mkoa wa Mwanza, Ukerewe n.k Serikali iangalie namna ya kupanua ofisi za utamaduni zisiishie ngazi ya Wilaya bali zifike katika ngazi za kata ambako kuna idadi kubwa ya watu wenye kuhifadhi vielezea vya utamaduni.

**MAREJELEO**

Akida, H. H. (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu Tanzania*. Dar es Salaam Printing House.

Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Research,* Belmont, Wadsworth publishing Company.

Balisidya, M. L. (1987). *Mulika Namba 19 Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi. Taassisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Bailey, K. D. (1994). *Methods of Social Reaserch*, Chikago, Maxwell Macmillan International.

Chesaina, C. (1991). *Images of Women in African oral Literature: Kalenjin and Maasai oral narratives as case studies*. Paper presented at Kenya Oral Literature Association Conference.

Cohen, L. na Lawrence, M. (2000). *Research Methods in Education,* London: Routledge.

Creswell, J. W. na Creswell, J. D. (2009). *Research Design, Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches.* Berrett-Koehler Publishers.

Denscombo, M, (2005). *The Good Reaserch Guide foa Small Scale Social Reaserch Projects*, New York, Open University Press.

Denzin, M. K. na Lincoln, Y. S. (2011). *The SAGE Handbook of Qualitative Research*. SAGE.

Deusi, G. S. (2011). Nyimbo za jando na unyago katika jamii ya Kikaguru kata ya Gairo, Morogoro. (Tasnifu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.Finnegan, R. (1976). *Oral Literature in Africa*, Oxford University press, Oxford.

Herbert, L. (2001). *Vitendawili vya Kabila la Kimatengo*, Chuo Kikuu cha Dar -Es - Salaam.

Kahn, J. A. (2011). *Research Methodology*, APH Publishing

Khairo, G. K. (2002). *Fani na Maudhui Katika Vitendawili vya Jamii ya Kiha.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kipury, N. (1983). *Oral literature of the Masaai.* Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

Kitundu, N. J. (2012). *Usawiri wa Wahusika Wanawake Katika Ngano za Kinyiramba*, Tasnifu, M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kombo, D. K. na Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *An Introduction,* Nairobi, Pauline's Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, methods and techniques.* New age international (p) publisher.

Kumar, R. (2010). *A step-by- step Guide for Beginners*. SAGE. Australia.

Kumar, R. (2013). *Research Methodology A Guide for Researchers in Agriculture Science, Social Sciences and other Related Fields.* Springer link- Bucher.

Leary, M. R. (2001). *Introduction to Behavioral Research Methods*. Allyn and Bacon, London.

Makala ya semina ya umoja wa waandishi wa vitabu Tanzania (1993). *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam University Press.

Makene, B. (2004). *Maudhui ya Vitendawili Katika Jamii ya Wajita*. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mbiu, C. (2013). Usawiri wa mwanamke katika ngano za kisambaa, Tasnifu, M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Mbughuni, P. (1983). *Riddles for thought*. Taarifa ya TUKI, Dar -es -Salaam.

Mgogo, Y. P. (2012). Utanzu wa ushairi: Matumizi ya nyimbo za Wanyiha Misibani. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, (Tasnifu M.A Kiswahili).

Mlacha, S. A. K. na Hurskainen, (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, Taasisi Ya Uchunguzi Wa Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam, Dar es Salaam.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Education Publishers and distributors ltd, Kibaha

Muhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1989). *Mulika Namba 21 Tanzu za Fasihi Simulizi*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili, OSW 105*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.

Mwansoko, H. J. (1998). *Mbinu za Uchambuzi wa Vitendawili*, Mulika namba 20, Jarida la TuKI, Dar es Salaamu

Ndalu, A. E. (1993). *Mazoezi na Marudio kwa Vyuo vya Ualimu. East African Educational Publishers.Nairobi*.

Ndalu, A. E. na Ikambili, H. M. (1991). *Kamusi ya Vitendwili na Mafumbo. Nairobi Kenya*. Thecreative print house limited.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1996). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*, Nairobi. University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Nicholaus, N. (2011). *Usawiri wa Kijinsia Katika Vitendawili vya Jamii ya Vwasu*, Tasnifu, M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Ph.D Thesis**,** Augustana College,Rock Island, IL.

Organisation for Social Science Research in Eastern and Southern Africa (2006). *Gender Issues. Research Report Series No. 23.* Printed in Ethiopia

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature; Background, Character and Continuity,*

Patton, M. Q. (2002). Qualitative Research & Evaluation Methods, SAGE Publications, Bloomington and Indianpolis. Indiana University Press.

Saussure, de Ferdnand. (1974) *Course in General Linguistics,* London: Fontana.

Seidman, I. (2015). *Interviewing as Qualitative Research: A Guide for Researchers in Education and the Social Sciences, 4th Ed.* Teachers College Press.

Sengo, T. S. Y. na Kiango, S. D. (1977). *Hisi Zetu.* Taasisis ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. na Kiango, S. D. 1977). *Fasihi Simulizi Vitendawili*, TUKI Dar -Es - Salaam.

Sengo, T. S. Y. na Kiango, S. D. (1985). *The Indian Complex and the Kiswahili Folklore: The Case of Zanzibarian tale-Performance*. Thesis submitted in fulfillment of the requerements for the degree of a doctor of philosophy (P.H.D folklore) of the University of Khoutum.

Sengo, T. S. Y. na Kiango, S. D. (2009). Fasihi za Kinchi, Dar es Salaam, AERA Kiswahili Researched, Products.

Senkoro, F. M. K. (1982). *Fasihi,* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Senkoro, F. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Senkoro, F. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki,* Dar es Salaa Universty Press: Dar es Salaam.

Senkoro, F. M. E. K., (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi Andishi", katika, *Kioo cha Lugha,* Juzuu 4. Idara ya Kiswahili, CKD. UK. 22-38: Dar es Salaam.

Senkoro, H. J. (1985) Vitendawili katika jamii maana, maudhui na matumizi yake. Mulika namba 17, TUKI Dar es Salaam.

Sevenye, W. C. and Robinson, R. (2001). *Qualitative Reaserch Issues and Methods, An Introduction for Educational Technologists,* USA, Arisona.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (2002). *Fasihi simulizi ya Mtanzania vitendawili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2007). *Makala ya kongamano la kimataifa Kiswahili 2000.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam

Wafula, R. M. and Ndungo, C. (1993). *BSW 308, Nadharia ya fasihi simulizi*. University of Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi. Focus Publication.

# VIAMBATANISHI

## KIAMBATANISHI A. MASWALI YA MAHOJIANO

Hojaji hii inalenga kukusanya vitendawili na kuchunguza usawiri chanya unavyojitokeza pamoja na ujumbe uliomo katika vitendawili. Mtafiti aliitumia hojaji hiyo wakati wa mahojiana na majadiliano kati yake na watafitiwa masikanini.

### Hatua ya kwanza

Taarifa za awali za watafitiwa, walijitambulisha kwa njia ya mdomo

Majina mawili…………………………………….…....…………………..

Umri(miaka)…………………………………………………..……………

Jinsia…………………………………………………………….……………….

Elimu…………………………………………………………………………….

Kijiji anachoishi………………………………...………………………….

Namba ya simu………………………………………………………………..

**B. Hatua ya pili (**Salaamu na utambulishi wa mtafiti)

- Kujitambulisha, jina, umri, historia ya maisha kwa kifupi

- Kutambulisha mada na madhumuni yake

### MASWALI YA UTAFITI

Maswali hayo yalijibiwa kwa njia mbili, maandishi kwa wale wenye uwezo wa kuandika, majibu mengine yalipatikana kwa njia ya mdomo na tuliyarekodi kwenye kilimbo maalumu kwa ajili ya uchambuzi

1. Unaelewa nini maana ya neno vitendawili (ivhili)……………………….………..

2. Jee, kwa nini watu husimuliana vitendawili (ivhili)……………….……………
3. Tega kitendawili(ivhili) chochote unachokijua kwa kutumia lugha ya Kinyiha
4. Jee, kitendawili (ivhili) hicho kinatoa mtazamo gani kuhusu mwanamke ?........
5. Kitendawili (ivhili) chako kinatoa mafundisho gani katika jamii yako…………

**KIAMBATANISHI B, VITENDAWILI VILIVYOKUSANYWA KUTOKA MASIKASNINI**

| VITENDAWILI KATIKA LUGHA YA KINYIHA | VITENDAWILI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI |
|---|---|
| 1. Inkaya yane yitali nu mlyango = Iji<br>2. Insiku zyonti kujenga ni kaya yane = Ingobe<br>3. Mumwitu twe vilu = Intenti<br>4. Untu umzelu akunanjizya pa mlyango =Insukusa<br>5. Kuluho lyitu twenti twevhafupi = Utukwii twa vibiriti<br>6. Zyungula uko nine inzyungule uku, tumfunye umpukupuku = Uvhugali<br>7. “Ubaba azenzile inyumba, yilinamaziho gavhili, iziho lyoka | nyumba yangu haina mlango = Yai<br>Siku zote natembea na nyumba = Kobe<br>Kwetu ni weusi = Chungungu<br>Mtu mweupe ana chungulia mlangoni = Kamasi<br>Ukoo wetu sote ni wafupi = Njiti za viberiti<br>Zunguka huko name nizunguke kule tumfundishe adabu = Jibu Ugali<br>Baba amejenga nyumba yenye vyumba viwili na sebule moja, chumba kimoja amelala mama, chumba cha pili amelala baba na sebuleni nimelala mimi. |

| | |
|---|---|
| akasite umayi, ilyamavho akasite ubaba, ane paperu. Navuluga igodo, kila mntu akwanza avhe wakuwandilo kumtwalila, apo inkonzye vhuli? (Jibu nkunyetula ivikombe vitatu ivhigodo, nkwinjila navyope kwa mayi, nkumleshela shoka, nkusyala navyo vivhili, nkusogola navyo kwa baba, nkumleshela shoka, sheshasyala kwepw nashope kusogola kumwela nene)<br><br>8. Umayi apafile avhana vhatatu vevhalingine = jibu Ifiga<br>9. Inga navhala kwa mwipwa | Nimeambiwa nitayarishe uji kwa ajili yangu mwenyewe na wazazi wangu (vikombe vitatu), lakini baba na mama kila mmoja anataka awe wa kwanza kupewa uji wake. Jee ni tatumia njia gani katika kugawa uji huo ili kila mmoja aridhike kuwa alipewa upendeleo? (Jibu, chukua vikombe vyote vitatu ingia katika chumba cha baba/ mama, unamwachia kimoja, unaondoka. Chukua viwili vilivyobaki, ingia navyo kwenye chumba cha pili, atakayepelekewa ataona umebeba vikombe viwili mkononi, ataamini kuwa amepewa nafasi ya kwanza, kimoja kitakachobaki utakunywa mwenyewe)<br>Mama amezaa watoto watatu wanaolingana = Jibu ni mafiga<br>Nikienda kwa mjomba sirudi = Jani/majani<br><br>shamba langu kubwa mavuno kidogo = nywele |

| | |
|---|---|
| ntakuwela = Itundu/amatundu | Nyumba yangu haina mlango = Yai/Kaburi |
| 10. Umugunda wane mpiti, nkuvuna ntehavhunsi = Insisi | |
| 11. Inyumba yane yitali numulyango = Iji/imbipa | Kuku wangu katagia mibani = Nanasi<br>Vilago ni vingi lakini ninalal chini - boga |
| 12. Inkuku yane yilasiye mmivwa = Inanasi | |
| 13. Ivilili ntevwawinji ilelo nkukata pansi = Ilyungu | Pita huku, nami huko, tumfinye mchawi = Ugali |
| 14. Tuha uku, nane ukwo, tumsine umulozi = Uwugali | Zunguka huko na mimi nizunguke huku tukutane katikati = Mkanda. |
| 15. Zyungula uko nine inzyungule uko tuhomane pakasi = Umsimbi. | Ndani mwetu wote ni weusi tiii = Chungu. |
| 16. Mumwitu twenty, twevhilu fiiii = Intente | Babu amevaa koti lakini ndevu ziko nje = Mhindi. |
| 17. Usokulu azwaye ikoti, ilelo indevu zili kunzi = ingagu. | Ndani mwetu tupo watatu akiondoka mmoja wote hatufanyi kazi = Mafiga |
| 18. Mumwitu tuhabha vatatu inga yepa woka twenti tutakubhomba imbombo = Amafiga. | Rafiki yangu ni mharibifu/mbaya lakini bado na mhitaji = Moto.<br>Nyumba yangu ina nguzo moja – Uyoga/Mwamvuli. |
| 19. Urafiki wane mnanjisu/mvhivhi ilelo kumwanza = Umwoto | Nyumba yangu ina mlango juu = Chupa |
| 20. Inyumba yane yilipanda lyoka = | |

| | |
|---|---|
| Uwoga/ Umwamvuli | Wazungu wanachungulia dirishaji = Kamasi |
| 21. Inyumba yane ilinumulyango kumwanya = Insupa | Ninapigwa faini bila kosa kulijua = Kujikwaa mguu |
| 22. Avhazungu vhakwinanjizya pidirisha = Nsukusa | Babu kalala ndani ndevu ziko nje = Mhindi. |
| 23. Nkuhomwa ishinangwa ntashimanyile = Kupunula ishinama | Mwalimu amekufa wanafunzi wanashangilia = Kinyesi na inzi. |
| 24. Usokolu akasite mnyumba indevu zilikunzi = Ingagu. | Huku mlima na huku mlima tarumbeta zinaria katikati = Mishuzi. |
| 25. Umwalimu afuye ilelo anvanafunzi nvakululuta= Ishivhozu ni nsanzi | Nivue nguo nikupe utamu - Ndizi |
| 26. Ukurigamba nukurigamba intaya zikukuta pakasi = Insuzi. | Babu anampiga bibi kila siku lakini bibi haondoki = Kinu na mche |
| 27. Nzura amenda, inkupe unvhunonu = Nkombwe | Koti la babu halikosi chawa – Nyota. |
| 28. Usokoru akuhomaga ubibi shima ilelo ubibi atakwepaga narumo = Ituri numnsi | Simama huko tumfinye mchawi = Ugali<br>Nyumba yangu ndogo wapangaji wengi = Kiberiti |
| 29. Ikoti ilyasokoru ritakuduraga impumi na rumo = Inzota. | Zunguka upenuni tumue bibi = Fito za kufungia nyumba |

| | |
|---|---|
| 30. Yimilila uko tumusine umulozi = Vhali | Nimejenga nyumba kwenye mtelemko = Sikio |
| 31. Inyumba yane yili na wapangaji avighinyi = Shibiriti | Ukoo wetu hauishiwi safari = Siafu. |
| 32. Zyungulila kuntanda tugoje unyohokulu = Lumango | Tajiri wa rangi = Kinyonga |
| 33. Nazenga inyumba yane palugalagata = Ikutwi | |
| 34. Uluho lwane hutakutuzya ukujenda = Nsalafu | Kila ninapokwenda anifuata = Kivuli |
| 35. Ine nedumbwe wa mavala = Ulumnvi | Mjomba hataki tuonane = Jani |
| 36. lwe kujenda akufyata mwasinda = Shinzunguli | Akienda kwa mjomba hawezi kurudi = Jani |
| 37. Umwipwa wane atakwanza tulolane = Itundu | |
| 38. Inga asogola kwa mjomba atakuwelaga = Itundu | Ukimchukua mama, beba na mtoto = Sagio |
| 39. Ingawanyetula unyina, utangaleha umwana = Ulwala ni nanyasyo . | Mama  anatembea na kibyongo = Konokono |
| 40. Umayi akujenda ni ng’ongo pansinzi = Inkozu | |

**Maneno mageni yaliyotumika katika utafiti huu**

| | |
|---|---|
| Aimanye | Aelewe vizuri |
| Fuzini | Mabega |
| Kongole | Pongezi |
| Igulu | Dari |
| Ishudu | Nyama ilikaushwa darini kwa kutumia moshi |
| Ivhili vya kusumba | Vitendawili |
| Makinika | Makini |
| Suluhu | Mapatano |
| Ufidhuli | Utovu wa adabu |
| Ulimbe | Sayansi |
| Ulitima | Shida, Shaka |
| Utangu | Kale |